
FEBRUARI MMXXV - TOLEO LA L

# NGURUMO
## ya Mwandishi




# MWEZI WA UPENDO

**HABARI KUU:**

•TUZO ZA KISWAHILI YA SAFAL YA FASIHI YA AFRIKA
Dirisha Lafunguliwa

## YALIYOMO

**TAHARIRI— Uk 02**
'FUNGA' KWA AFYA NA TOBA

**MWANDISHI WETU— Uk 03**
ALLY NASSORO PX

**NEW IN TOWN: Uk 04**
KIJASHO CHEMBAMBA

**PITIO LA VITABU— Uk 05**
CHUNGU TAMU—5

**SAIKOLOJIA: Uk 06— 07**
DHIBITI HISIA

**MAKALA: Uk 08 - 09**
UMUHIMU WA USOMAJI VITABU KWA WATO-TO

**KUTOKA KWA FANANI: Uk 10**
MAMBO KUMI NILOIYOJIFUNZA

**SAKO KWA BAKO – Uk 11**
SEBASTIAN MAPUNDA

**RIWAYA: Uk 12—13**
2080

**RIWAYA: Uk 14—15**
Najutia Kuwa Na Wewe '11'

**YA KALE NI DHAHABU: Uk 16**
SAFARI 7 ZA SINDBAD BAHARIA—01

**HABARI MOTO: Uk 17**
TUZO YA SAFAR CORNEL

**SHUBAKA LA VITABU: Uk 18**
NAGUIB MAHFOUZ

**KITABU NILICHOSOMA: Uk 19**
MY LIFE MY PURPOSE

**MATANGAZO: Uk 22**

**MALENGA WA KILEO: Uk 21**
KAMA MOSHI na FURAHA

**HABARI PICHA: Uk 20**

**KUTOKA MAKTABA: Uk 23**
HAMMIE RAJAB

**ELIMU JAMII: Uk 24 & 25**
SAFARI YA MALEZI (8): HATUA ZA MALEZI

**HADITHI: Uk 26 - 27**
K.O.K.W.A

**HADITHI: Uk 28 - 29**
NGUVU YA KIAPO '09'

**KALAMU YANGU : Uk 30 - 31**

KIROBA CHEUSI - LAURA PETTIE

## TAHARIRI:
## 'FUNGA' KWA AFYA NA TOBA

Nakusalimuni ndugu zangu,

Natumai nyote mu wazima kabisa na bukheri wa afya. Toleo letu la 50 limekujieni kwa kuchelewa kidogo kutokana na hitilafu za vifaa vyetu. Lakini twamshukuru sana Mungu kwa kuwa leo hii, li mikononi mwako.

Wapenzi wa Ngurumo ya Mwandishi, najua kuwa nyote mnajua kwamba huu mwezi wa pili ni wa pekee sana kwa sababu dini kubwa mbili duniani; yaani Wakristo na Waislam zinaingia katika mfungo wa Kwaresma na Ramadhani mtawalia. Sote tunajua vyema kwamba Kwaresma ni siku 40 za kufunga na kufanya toba na Ramadhani ni siku 30 za kufunga na kufanya toba.

Tukiwa kama wauminiwa dini hizi mbili, hatuna budi kufuata miongozo stahiki katika kufanya 'funga' zetu. Pamoja na kwamba tunatakiwa kufunga kama sehemu ya toba kwa makosa yetu lakini tujue kwamba mifungo hii ni wakati wa mazoezi ya kubadilisha mitindo ya maisha yetu. Twatakiwa kupunguza chakula tunachokula kila siku, kuachana na anasa nk. Lengo kuu ni kutufanya upya kuwa watu wapya mbele ya Mola wetu.

Lakini Pamoja na hayo yote, tunapaswa kutazama mifungo hii kwa upande wa pili, yaani kwa upandewa afya zetu. Siku hizi watu wengi tumekuwa na afya mbovu sana, tumekuwa wanene kupita kiasi, wavivu kupita kiasi na magonjwa kama sukari, presha yamekuwa ya kawaida sana kwetu, kwanini? Kwa sababu ya ulaji mbaya wa vyakula na maisha ya kivivu na anasa tunazoishi.

Kupitia mifungo hii ambayo yote inaanza tarehe 18 ya Februari, basi na tuunganishe toba zetu na kuboresha afya zetu. Iwe nafasi ya kufanya 'diet'. Tufanye mfungo-tiba hasa kwa wale ambao miili yetu imekuwa na uzito mkubwa ambao ama unatuletea magonjwa au umetuingiza kwenye magonjwa. Hebu tutumie mifungo hii hata kupunguza utazamaji wa luninga na matumizi ya simu ili miili yetu, nafsi zetu na roho zetu zipate muda wa ujitafakari na kujianza upya.

Nakutakieni Kwaresma na Ramadhani njema sana!

C.E.O - Richard Mwambe


**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## MWANDISHI WETU:
## ALLY NASSORO PX



**Katika toleo letu la 50, tunamkaribisha mwandishi Ally Nassoro Ngagesa. Mwandishi mbunifu anayefanya vizuri sana katika uga huu wa sanaa ya fasihi. Hapa Nassoro anaeleza kuhusu yeye mwenyewe na kazi yake.**
**Hebu basi, tumsome na tumjue!**



ALLY NASSORO PX

Jina langu naitwa Ally Nassoro Ngagesa, ila kwa jina la uandishi na sanaa kwa ujumla naitwa Ali Nassoro Px.
Ni mzaliwa wa Jiji la Dar es salaam ndani ya wilaya ya Temeke.
Elimu ya shule ya msingi niliipata katika Shule ya Msingi Mabatini iliyopo, Tandika maghorofani baadae nikahamia Kiburugwa iliyopo Mbagala, Dar es salaam.
Baada ya hapo nikapita Shule ya Sekondari kingugi na kumalizia elimu yangu ya chuo kikuu Zanzibar katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume.

**Kwanini napenda kuandika**
Kwanza, naomba ijulikane kuwa nina mahaba kindakindaki na uandishi, yumkini kama uandishi ungekuwa pombe basi ningekuwa *mlevi-mbwa*.
Napenda sana kusoma na kuandika kidogo tu.
Napenda kuandika kwa sababu nimechagua uandishi kuwa ni miongoni mwa sehemu yangu ya maisha. Kwangu uandishi ni kama maji haiwezi kutimu siku pasi na kuandika au kusoma kitu chochote kile.

**Faida za uandishi**
Kwa upande wangu uandishi unanipa furaha na amani ya nafsi yangu. Japo kuwa nina imani ipo siku uandishi utanipa kitu cha ziada zaidi tofauti na furaha na amani ya nafsi.

**Changamoto za uandishi**
Changamoto ninazozipitia mimi sio kubwa sana japo kuwa inawezekana zikawa kubwa kwa wengine.
Changamoto kuu hasa ni;-
**Ukosefu wa bajeti ya uandishi:** Mwandishi chipukizi anapoanza kuandika, uwa huona uandishi ni kazi nyepesi mno, ila kila anavyozidi kuandika ndipo anagundua kuwa kazi ya uandishi ni ngumu na inahitaji bajeti ya fedha au vifaa ili kupata kazi bora yenye viwango stahiki.

**Kutoelewa na kutokuwa na takwimu sahihi zasoko la fasihi andishi**
Kama Mwandishi nashindwa kujua na kuelewa muelekeo wa ukuaji wa fasihi andishi nchini, nashindwa kuelewa wanafasihi kipi hasa wanachohitaji kwa sasa, nashindwa kufahamu ni kazi zipi zinauzika zaidi kwenye fasihi andishi.
Lakini pia nakosa takwimu za mauzo za kazi za kifasihi kila mwandishi anasema yeye kauza zaidi kuliko mwingine.

**Ukosefu wa muda**
Changamoto kubwa kwenye uandaaji wa fasihi andishi ni muda, mwandishi anakuwa yupo kwenye dunia ya peke yake ambayo haitaji mtu mwingine aingie au amtoe kwenye hiyo dunia kama yeye mwenyewe hajawa tayari kutoka.
Hii inapelekea mizozano na mikwaruzano ya kila mara na watu wa karibu ambao mara nyingi wanahitaji muda na ukaribu wangu kila mara.
Mbaya zaidi wengi utafsiri kama dharau ila kiuhalisia sio dharau wala si kuweka muda wa michepuko.

Mpaka sasa bado sijachapa kitabu, kitabu/ vitabu ila panapo majaaliwa mwaka huu Mwenyezi-Mungu akijaalia kazi yangu ya kwanza itachapishwa na kupitia kurasa zangu za mitandao ya kijamii wanafasihi watapata taarifa za ujio wa kitabu changu cha kwanza kabisa.

Malengo yangu kama mwandishi kuwa miongoni mwa magwiji wa fasihi andishi nchini na duniani kwa ujumla, pesa kiwe kitu cha ziada lakini lengo kuu hasa natamani kuona mtu au watu wanabadilika au wanajifunza kitu kutokana na maandiko yangu.

**Jinsi ya kuzipata kazi zangu**
Kwa sasa njia rahisi zaidi na nyepesi ambayo mwanafasihi ataitumia kupata kazi zangu, ni kufatilia na kuwa karibu zaidi na kurasa zangu za mitandao ya kijamii hasa zaidi kurasa ya mtandao wa Facebook (*Ali Nassoro Px)*
Nina aimani mwanafasihi atafurahi, atajifunza na kuwafunza wengine kupitia maandiko mbalimbali yaliyojaa kwenye ukurasa wangu wa Facebook.

## KITABU KIPYA MJINI

## KIJASHO CHEMBAMBA

Shamila Filbert ni binti mrembo na mwanafunzi wa chuo nchini Madagascar ambaye maisha yake yanageuka kuwa jehanamu baada ya mpenzi wake kumwacha na kuoa mwanamkemwingine. Kwa hasira na uchungu, Shamila anafanya uamuzi mbaya anamkodisha muuaji wa kulipwa ili akaharibu ndoa hiyo, lakini mpango huo unamgeukia na kuwa laana.

Mambo yanaharibika zaidi pale mdogo wake, Izack, anapojaribu kumsaidia kwa kudukua (kuhack) mifumo ya chuo.

Kitendo hicho kinasababisha Shamila akamatwe mbele ya watu na kujulikana nchi nzima kama Mdukuaji wa Chuo Kikuu.

Mahakama inamuhukumu kifungo cha miaka 30 jela na kutaifisha mali zote za familia yake ikiwemo biashara ya mama yake ya ASHA BEAUTY EMPIRE na nyumba yao ya kifahari kama faini ya dola milioni 300.

Akiwa gerezani, pigo lingine linatokea wazazi wake wanauawa kwa bomu wakiwa ndani ya msikiti wa Masjid Al-Akbar kutokana na visasi dhidi ya baba yake.

Ili kumwokoa na hukumu ya kifo, askari mmoja anayeitwa Mike anampa ujauzito na kumtorosha gerezani.

Shamila anajificha kwenye meli ya mizigo akiamini anakwenda Msumbiji, lakini anakumbana na ukatili wa wafanyakazi wa meli hiyo wanaotaka kumuua na kumtupa baharini. Kwa miujiza, anafika jijini New York, Marekani, ambako anaangukia kwenye genge moja hatari.

Fungua kurasa za kitabu kitabu hiki, ujue hatima yake.

VITABU VITAPATIKANA DAR ES SALAMA MAENEO YAFUATAYO.

Kinondoni Moroco, Duka la Kona ya Riwaya Kwa Zamira 0655428085.

Dar es salama Posta Mpya kwa George Kalambo karibu na Sanamu la Askari.

0755454152.

Magomeni Kwa Molito Duka la Kalamu Tulivu Bookshop 0718975659.

Usiwaze kuhusu usafiri. Kama upo Dar es Salaama, nakuletea kitabu mpaka mlangoni kwako BURE KABISA.

KWA NDUGU ZETU WA MIKOANI

Je, unakitaka haraka? Lipia Tsh 8,000 tu ya usafiri na mzigo utatumwa kwako mara moja na kukufikia popote ulipo Tanzania..

NAMNA YA KULIPIA

Fanya miamala yako kwa usalama kupitia




HALOPESA 0637383623

JINA ISSA RAMADHAN ISSA.

WASILIANA NAMI MOJA KWA MOJA

WhatsApp 0760458050

Call /SMS: 0742128452.

# Diwani - CHUNGU TAMU (5)



**DIWANI YA CHUNGU TAMU**

**MWANDISHI: THEOBALD MVUNGI**

**WACHAPISHAJI: TPH**

**MWAKA: 1985**

**Inatoka toleo lililopita…**

**4. KUWEPO NA EMOKRASIA YA KWELI**

(….)"Barani mabavu yatumika,

Dikteta asijeanguka,

Na majungu pia ayapika,

Udikteta pasi shufaka,

Nasimulia ya Afrika

Mwandishi anaonesha kuwa mabavu yanatumika ili kumlinda dikteta asije akaangushwa kwa kufuata mfumo wa demokrasia ya kweli.Madikteta hao hutumia vyombo vya dola kama vile polisi, jeshi,magereza na mahakama ili kutetea maslahi yao.Kwa ujumla anatoa pendekezo kuwa, ili tuweze kujenga jamii mpya hatuna budi kujenga na kudumisha demokrasia ya kweli katika harakati zetu za maisha.

**5.KUPIGA VITA MATABAKA**

Matabaka ni hali ya watu kuishi kufuatana na madaraka walionayoya,uchumi na siasa n.k.Msanii ametumia vielelezo halisi kufikisha ujumbe kwa jamii.Katika shairi la "Wimbo wake Hotubani" mwandishi anasema;

*Magavana majimboni, wasambazao nchini,*

*Wapewa kubwa idhini, na watune ofisini,*

*Wasoingia shambani, Kwa sifa madarakani.*

Mwandishi anadhihirisha matabaka yaliyopo nchini mwetu. Magavana wanawakilisha tabaka la juu (viongozi) na punda na ngamia wamechorwa kitaswira kuwakilisha wananchi wanyonge wanaoteswa na kunyanyasika.

Katika shairi la *"Wengi Wabaki Taabuni"* mwandishi anasema;

*Mesikia kilio gizani,*

*Jamaa apita njiani,*

*Ghafla akakabwa kooni,*

*Kapigwa kabari ya kihuni,*

*Yaitwa demokrasi guni.*

Mwandishi anaonesha kuwa, kuna matabaka ya aina mbili katika jamii yaani tabaka la wachache wanaofurahia maisha na tabaka la wengi wanaoteseka taabuni.


Kwa ujumla mwandishi ameonesha kuwa mgawanyiko wa watu katika matabaka huleta utengano katika jamii. Ili tuweze kufaulu kuijenga jamii mpya (endelevu) hatuna budi kupiga vita matabaka yaliyoshamiri katika jamii. Lengo liwe kuijenga jamii yenye kufuata misingi ya haki na usawa.

**6. KUEPUKA VITA (UHASAMA)**

Vita husababisha uhasama katika jamii. Huleta ugomvi na kutokuelewana miongoni mwa watu.Vita hurudisha nyuma maendeleo ya jamii.Vita huleta athari mbaya katika jamii. Mfano vifo, umasikini, ugumu wa maisha. Katika shairi la *"Tishio la Binadamu"*, mwandishi anasema:-

*Mashindano ya silaha, yamekuwa ni mchezo,*

*Wakubwa waona raha, kwa silaha waziundazo,*




*Mabomu yaso na silaha, ndiyo yanawapa uwezo,*

*Urusi na Marekani, dunia mwaipa adha"*

Mwandishi anaitahadharisha dunia kuwa vita kuu vinanukia. Hii ni kutokana na uhasama uliopo kati ya nchi na nchi pamoja na utengenezaji wa silaha kali kutoka Urusi na Marekani. Kutokana na hali hii dunia nzima sasa iko mashakani juu ya vita. Mwandishi anaendelea kueleza kuwa mashindano ya silaha yamekuwa ni mchezo na nchi kubwa zinaona fahari kuzitengeneza.

**Itaendelea toleo lijalo...**



+255 763 013 206.
MADAM NEEMA MGAO,
DODOMA,

**DHIBITI HISIA**

Habari ya wakati huu, hongera kwa kuvuka mwaka, kila wakati utumie kumshukuru Mungu kwa kukuvusha hadi kuuona mwaka huu, si unaona wewe mwenyewe kuwa kwa tikitaka ulizozipiga mwaka 2025 pengine wewe kuwa hai mpaka hii leo ni neema na kudra za Mungu tu, lakini kiuhalisia haustahili? Basi mwaka 2026 tuutumie kwa kuishi vizuri na kutenda yaliyo mema. Ikiwa tutatenda dhambi tusiache kutubu kwa Mungu. Tusiache kutendea mema wengine. 2026 tusiache kuishi vizuri, na tuishi vizuri pia na wale watuzungukao.

Mwaka 2026 tumeuanza, katika jarida hili la NGURUMO YA MWANDISHI, kwenye uwanda huu wa makala za saikolojia na tuanze kwa kupata elimu ya namna ya kudhibiti hisia. Wengi wameingia matatizoni au wamefanya mambo ya ajabu wakati mwingine kupelekea kumkosea Mungu na binadamu wengine.

**HISIA NI NINI?**

Hisia ni mawazo ya ndani mwa mtu.
Hisia ni mrundikano wa fikra za ndani.
Hisia ni mchemko wa fikra za ndani kwenye moyo na akili ya mtu zinazozalishwa na eidha hasira au furaha katika moyo au fikrani mwa mtu.

Siku moja nilifanya uchunguzi, nikamchukua mtu aliyekua na furaha sana, kiasi cha yeye kuwa anaruka ruka kutokana na furaha ile, na nikamchukua mtu mwenye hasira sana kiasi cha yeye kutetemeka kwa hasira. Nikagundua kuwa wote wawili katika kiwango cha hisia walizonazo wanaweza kufanya mambo makubwa sana ambayo pengine yataleta matokeo hasi au matokeo chanya.

Nikagundua kuwa watu wote wawili, kwa nyakati hizo walizonazo, wanaweza kufanyiwa kitu na wasisikie muitikio ndani ya miili yao kwa uharaka. Kwamba, ikiwa yule mwenye furaha kupitiliza, ukimkata na kisu sehemu yoyote ya mwili wake itamchukua dakika moja ili kuirudisha akili kuwa sawa na ikapokea maumivu yale ya kukatwa. Vivyo hivyo kwa mtu mwenye hasira kali, itamchukua dk 3 kujipooza hasira kisha kupokea maumivu na ama kuirudia hasira yake au kupoa ili kuishusha hasira zake.

**NINI HUSABABISHA KUPANDA NA KUSHUKA KWA HISIA**

Hisia husababishwa na vichocheo fikra vilivyopo ndani ya mwanadamu husika. Ikiwa atafanya au kufanyiwa jambo la kufurahishwa basi *homones* zinazohusiana na uchochezi wa hisia za furaha kuzaliwa. Zitafanya kazi kwa kasi, na ndani ya sekunde 20 zitaanza kupandisha hali ya furaha kupitiliza. *Homones* hizo huendelea kujichochea na kuendelea kujizalisha kwa wingi na hivyo kufanya furaha kuongezeka mpaka kufikia kuuteka ufahamu na mwili wa mhusika na kufanya asisikie wala kupata kupokea hali mpya.

Vivyo hivyo na kwa mtu mwenye kutawaliwa na hisia za hasira, sekunde 20 zinatosha kwa uchochezi wa *homones* zinazozalisha hali ya hasira, na taratibu hasira huendelea kupanda mpaka kufikia kupandwa kwa hasira kwa kiwango kikubwa kiasi cha kushindwa kujizuia kushusha hasira kwa muda husika.

## Dhibiti hisia zako

Inawezekana kuwa wewe au mwenza wako, ndugu, rafiki yako ni moja kati ya wahanga wa matukio yasababishwayo na kushindwa kudhibiti hisia. Tuone

## DHIBITI HISIA

hatua au mambo machache yanayoshauriwa kufanywa ili kudhibiti hisia.

**FANYA IBADA**

Hasa hasa wale ambao wakikasirika na akili huruka, unashauriwa kuwa karibu sana na Mungu. Daima muda wote uwe mtu wa kutenda mema na kuepuka kupokea kuzalishiwa au kujizalishia hasira.

**JIFUNZE KUJIPIMIA/ KUJIPA KIASI**

Iwe ni hisia za kufurahi au hisia za kukufanya uchukie, aina yoyote ya hisia zinazokutesa, unashauriwa kujifunza kujipimia au kujipa ukomo, jipe kiasi katika kufurahi na ujipe kiasi katika kuchukia pia. Hali zote mbili huzaa tabia, tabia ambazo ndizo huwa mazoea na kuwa na uwezo wa kujiumbia tabia mpya kila wakati hivyo unashauriwa kujiumbia na kujipa kiasi kwa hali zote.

**JIZUNGUMZISHE**

Ikiwa umekasirika sana, badala ya kupanga mipango ya kufanya madhara Zaidi unashauriwa kujizungumzisha ili kujipa kujizuia katika kukasirika zaidi. Wakati wowote jipe muda wa kuisikiliza ile sauti ya ndani inayokuonya ama kufurahi sana au kuchukia sana.

**HAMA SEHEMU**

Uonapo kuwa inaweza kutokea madhara makubwa kuendelea kubaki pahala hapo ambapo pamekuzalishia hasira au furaha kupitiliza, maana kuna mwingine akifurahi ni mpaka alie, wakati mwingine kulia lia mbele za watu ni udhaifu. Uonapo kwamba kuendelea kubaki hapo kunaweza kuendelea kukuzalishia hasira au furaha zaidi unashauriwa kuhama eneo hilo. Hii iwafae hasahasa wanandoa ambao wanasumbuliwa na ugomvi kila mara, ukiona unahasira kwa kiasi cha kutaka kupiga mkeo au kumdhuru mumeo basi unashauriwa kuhama kabisa eneo hilo ili kujishusha hasira yako.

Wengi wamejisababishia madhara makubwa kwa kushindwa kudhibiti hisia zao za ndani, wapo waliopata kuzamia katika kusababishiwa kesi kutokana na hasira na kushindwa kujidhibiti. Wapo waliofungwa kutokana na kuleta madhara katika jamii kwa kushindwa kujidhibiti. Wapo waliowapa ulemavu wapendwa wao kwa kushindwa kujizuia na kujidhibiti hisia zao hata zikaleta madhara.

Mwaka 2026 Kataa kupelekeshwa na hisia, furahi lakini furahi kwa kiasi, chukia lakini chukia kwa kiasi.

**HAPPY NEW YEAR. MUNGU NA ATUBARIKI NA KUTUFANIKISHIA MAMBO YETU**

Karibu kupata huduma za ushauri wa kisaikolojia na kupata vitabu vya kisaikolojia. **JITIBIE KISAIKOLOJIA… TSH. 15,000 -** Hiki ni tiba ya kisaikolojia kwa mambo yote yatuzungukayo. , kiitwacho **SAIKOLOJIA YA MAHUSIANO NA NDOA… TSH.10,000** - Hiki ni kitabu kingine kwa ajili ya walio kwenye ndoa na mahusiano.
Na hivi sasa kwa mwaka huu 2026, nimeingiza kitabu kipya cha riwaya kinachomhusu mwanamama GABEDA, kitabu kiitwacho GABEDA.

KWA HUDUMA ZOTE WASILIANA NAMI KUPITIA WHAT'S APP AU SIMU YA KAWAIDA +255 763 013 206.
MADAM NEEMA MGAO,
DODOMA,
TANZANIA,
+255 763 013 206.



**Je; unataka kuhaririwa, kuandikiwa (ghost writing), kuhakikiwa au kuchapiwa hadithi au kitabu chako?**

**Wasiliana nasi kwa**
**Whatsapp: 0766974865**
**Call: 0672160016**

**Gharama zetu ni nafuu mno… mpaka mwenyewe utashangaa…!**

MAKALA

Na. Richard Mwambe

# UMUHIMU WA USOMAJI VITABU KWA WATOTO

Kujenga utamaduni wa kusoma kwa watoto ni moja kati ya zawadi bora zaidi unazoweza kuwapa. Sio tu kuhusu ufaulu wa shule, bali ni kufungua milango ya ubunifu na maarifa yatakayowasaidia maishani mwao kote. Siku hizi Watoto wengi wamekuwa wakijifunza mambo mbalimbali kupitia luninga na simu. Mambo hayo, asilimia kubwa yanaenda kinyume na tamaduni za Mwafrika/Mtanzania. Hii yote inatokana na wazazikutothamini usomaji vitabu katika familiazao. Katika Makala hii tutaangazia mbinu Watoto wapende kusoma vitabu. Zaidi tutatazama falsafa ya usomaji vitabukwa Watoto.

**Hapa kuna mbinu bora za kuwafanya watoto wako wapende vitabu:**

## 1. Kuwa Mfano wa Kuigwa (Role Model)

Wazazi mnapaswa kuwa mfano wa kuigwa na Watoto wenu. Watoto ni kama kioo; mara nyingi hufanya kile wanachokuona ukifanya, si kile unachowaambia wafanye.

* **Soma mbele yao:** Badala ya kushinda kwenye simu au TV, chukua kitabu au gazeti na usome.

* **Onyesha furaha:** Waonyeshe kuwa kusoma ni kitu unachofurahia, si kazi ya kulazimishwa.

**2. Anza Mapema** (Hata Kabla Hawajajua Kusoma). Huna haja ya kusubiri mtoto aanze shule ili aanze kuwa na urafiki na vitabu.

* **Wasomee hadithi kila siku:** Dakika 10 hadi 15 kabla ya kulala ni muda mzuri wa kutengeneza ukaribu na vitabu.

* **Vitabu vya picha:** Kwa watoto wadogo sana, tumia vitabu vyenye picha nyingi na rangi za kuvutia.

## 3. Tengeneza "Kona ya Kusoma"

Mazingira yana ushawishi mkubwa katika tabia ya mtoto.

* Weka rafu ndogo ya vitabu inayofikiwa na mtoto kwa urahisi.

* Tengeneza sehemu yenye utulivu, mto laini, na mwanga wa kutosha ambapo mtoto anaweza kukaa na kusoma kwa raha.

## 4. Waache Wachague Wanachopenda

Kulazimisha kitabu fulani kunaweza kumfanya mtoto achukie kusoma.

* **Gundua vipaji vyao:** Kama mtoto anapenda wanyama, mpe vitabu vya wanyama. Kama anapenda magari au anga, mtafutie vitabu hivyo.

* **Tembelea maktaba au duka la vitabu:** Mpeleke mtoto na umwache ajichagulie kitabu anachovutiwa nacho.

### 5. Fanya Kusoma Kuwe ni Mchezo, si Adhabu

Kamwe usitumie "kusoma kitabu" kama adhabu ya kosa alilofanya mtoto. Badala yake:

* **Tumia sauti tofauti:** Unapowasomea, badilisha sauti kulingana na wahusika (mfano: sauti ya simba, sauti ya sungura).

* **Uliza maswali:** "Unadhani nini kitatokea baadaye?" Hii inamsaidia mtoto kutumia akili yake kufikiri.

## Yafuatayo ni mapendekezo ya umri wa mtoto na kitabu cha kusoma:-

Miaka 0-3 anatakiwa kusoma vitabu vya picha, vitabu vya vitambaa/plastiki. Lengo kuu hapa ni kutambua rangi, vitu, na sauti. |

Miaka 4-6 anatakiwa kusoma hadithi fupi zenye maneno machache na picha nyingi. Lengo kuu ni kujifunza herufi na sauti za maneno.

Miaka 7-10 anapaswa kusoma vitabu vya hadithi ndefu *(Chapter books),* katuni. Lengo ni kujenga uwezo wa kuelewa na kufuatilia mtiririko.

Miaka 11+ anapasswa kusoma riwaya za vijana, vitabu vya maarifa, wasifu. Lengo kuu ni kujenga mtazamo na uchambuzi wa mambo.

**Kidokezo cha Dhahabu:** Punguza muda wa vifaa vya kielektroniki *(Screen time).* Ni vigumu kwa kitabu kushindana na michezo ya

video au katuni za TV kama mtoto hana mipaka ya matumizi ya vifaa hivyo.

Falsafa ya mtoto katika kusoma haihusu tu uwezo wa kutamka herufi, bali ni jinsi anavyohusiana na ulimwengu, maarifa, na nafsi yake. Mtoto hazaliwi akijua kusoma, bali anazaliwa akiwa na shauku ya asili ya kugundua.

## Falsafa ya Usomaji wa Vitabu kwa Watoto

Tunaweza kuigawa falsafa hii katika misingi mikuu minne:

1. **Kusoma kama Ugunduzi** *(The World as a Map)*

Kwa mtoto, kusoma si kazi *(labor),* bali ni *adventure*. Falsafa hapa ni kwamba kitabu ni dirisha linalomruhusu kuona maisha ambayo hajayafikia bado.

* **Mtazamo wa Mtoto:** "Kitabu kinaniambia nini kuhusu dunia?"

* **Lengo:** Kutosheleza udadisi wake wa asili *(Natural Curiosity)*.

2. **Kusoma kama Utambulisho** *(Mirror and Window)*

Falsafa hii inasema kuwa mtoto anasoma ili ajione yeye mwenyewe *(Mirror)* au awaone wengine *(Window)*.

* **Mirror (Kioo):** Mtoto hutafuta wahusika wanaofanana naye (wenye rangi yake, lugha yake, au changamoto zake) ili ajihisi ana thamani.

* **Window (Dirisha):** Mtoto hutafuta kuelewa watu walio tofauti naye ili ajenge huruma na uelewa *(Empathy)*.

**3. Falsafa ya "Tabula Rasa" na Ujenzi wa Maana**

Ingawa nadharia ya zamani ya Tabula Rasa (ubongo mweupe) inasema mtoto hajui kitu, falsafa ya kisasa ya elimu *(Constructivism)* inasema mtoto anajenga maana.

* **Mtoto hasomi tu maneno;** anachukua kile alichosoma na kukichanganya na vitu anavyoviona nyumbani au mtaani.

* **Mfano:** Akisoma kuhusu "urafiki" kwenye kitabu, anaanza kutathmini urafiki wake na watoto wenzake uwanjani.

### 4. Kusoma kama Uhusiano wa Kihisia (Emotional Connection)

Hapa ndipo falsafa ya "Kusoma ni Upendo" inapokuja. Kwa mtoto mdogo, kusoma kunahusishwa na muda wa mzazi.

* Kama unasoma naye huku umemkumbatia, falsafa yake inakuwa: "Kusoma = Usalama na Upendo."

* Kama kusoma kunatumika kama adhabu, falsafa yake inabadilika kuwa: "Kusoma = Maumivu na Shinikizo."

## Tofauti ya Falsafa: Mtoto vs. Mtu Mzima

Wakati mtoto anaposoma kitabu daima hutaka kujua kitu na kufurahi, mtu mzima akisoma kitabu hutafuta suluhisho la tatizo.

Wakai mtoto husoma kwa kujali hadithi na picha, mtu mzima hujali kumaliza na kupata ujumbe fulani

Wakati mtoto huona kuwa kitabu ni mwanzo wa mcjezo wa kuagiza, mtu mzima huona kitabu ni hitimisho la mada Fulani.

## Hitimisho la Kifalsafa

Falsafa bora ya kumjengea mtoto ni ile ya "Msomaji Huru". Hii inaamini kuwa mtoto ana haki ya:

* Kuchagua anachotaka kusoma.

* Kuacha kusoma kitabu kama hakivutii (kama watu wazima wafanyavyo).

* Kusoma kitabu kile kile mara 100 (marudio hujenga usalama na uelewa wa kina).

R.M.

## Asemavyo AMOSI BWIRE 'BABA BM'
## MAMBO 10 NILIYOJIFUNZA BAADA YA KUTOA RIWAYA YANGU YA KWANZA:

1. Usikurupukie uchapaji wa kitabu, kabla ya kufanyiwa uhariri na uhakiki wa kutosha. Kubali kuingia gharama ya kupata mhariri au mhakiki mwenye uwezo ili kupunguza kasoro za kiuandishi (Kitabu kinapokuwa na makosa mengi ya kiuandishi kinafanya wasomaji wasikipende, hata kama kina simulizi ya kuvutia kiasi gani).

2. Kuwa mtaaalam wa matangazo hakukupi uhakika wa kuweza kuuza nakala nyingi za kitabu (unaweza kukitangaza sana kitabu chako siku za mwanzo na watu wakakinunua, lakini bunde baada ya kukisoma unaweza kushagaa wamegeuka kuwa wapondaji wako wakuu, kiasi cha kugeuka kuwa nuksi mbeleni, badala ya mtaji sokoni).

3. Wiki chache za kwanza baada ya kutoa kitabu chako ni za muhimu sana kwako kukitangaza kitabu chako kwa nguvu na mbinu zote (ni ngumu kutangaza kitabu mwaka au miaka baada ya kukitoa, labda kiwe na ubora wa kipekee).

4. Kitabu kimoja kizuri hakiwezi kukupa mafanikio makubwa sokoni. Bali kitakuwa ngazi ya kuwafanya wasomaji wakuamini na kununua vitabi vyako vingine, jambo litakalopekelea kupata mafanikio sokoni (Unapaswa kutoa vitabu kadha wa kadha ili kufikia malengo ya kipato uliyokuwa nayo awali, sio kutegemea kitabu kimoja pekee).

5. Ukiandika kitabu kizuri jitahidi kutokaa muda mrefu kabla ya kutoa kitabu kingine (wasomaji hawana kumbukumbu za muda mrefu, ukiwakalisha sana wanakusahau!).

6. Usitegemee msisimko mkubwa toka kwa watu siku ya uzinduzo wa kitabu chako. Msisimko utakuja baada ya wewe kukitangaza na watu waliokisoma kukisifia (usikatishwe tamaaa na mapokeo ya wawali ya kitabu chako. Hayana nafasi kubwa kwenye mafanikio yako kama utakuwa umewagusa watu waliokisoma na wakaamua kukupa sapotiya dhati).

7. Hata uandike kitabu bora kuliko vyote duniani, kuna mtu au watu watakaokichukia na kukiongelea vibaya kwa wengine (Usijiaminishe kuwa ni lazima kila mtu akipende kitabu chako. Kila kitabu kina watu wake. Hakuna kitabu kilichoandikwa kwa ajili ya kila mtu).

8. Kuandika kitabu kizuri pekee sio kigezo cha kupata mafanikio makubwa sokoni (uwezo wako wa kuandika hauna uhusiano wa moja kwa moja na uwezo wako wa kuuza vitabu. Kuna mambo mengi yanayochangia mafanikio ya kitabu sokoni, zaidi ya ubora wa uandishi).

9. Usanifu wa jalada la kitabu chako unachangia kwa asilimia 50% kwenye mafanikio ya kitabu chako sokoni (jitahidi kutumia wataalamu sahihi na muda wa kutosha kusanifu jalada la kitabu chako, ni muhimu sana!)

10. Ridhika na kazi yako. Hakuna mtu atakayekuja kukufanya uifurahie au uridhike na kazi yako, zaidi yako wewe mwenyewe. Kubali makosa yako ili ujiboreshe, na furahia ubora wako ili usijikatie tamaa). Kumbuka; kuna vitabu vipya zaidi ya 10,000 vinatolewa kila siku Duniani, na vitabu zaidi ya milioni mbili (2,000,000) hutolewa kila mwaka Duniani. Sherehekea kuwa mmoja wa hao watu Elfu Kumi tu waliotoa kitabu siku hiyo, na milioni mbili waliotoa kitabu mwaka huo.



# SAKO KWA BAKO:

## SEBA MA: 'TUSOME VITABU KWA AFYA'

**Jina langu ni Sebastian Mapunda, naishi Mkoa wa Ruvuma, wilaya ya Mbinga.**

**Ni kitu gani hasa kilikufanya uwe msomaji wa vitabu?**
Mpangilio wa matukio katika Simulizi aina ya Simulizi kwa sababu Mimi ni mpenzi wa Simulizi za Action/ kijasusi

**Hebu tujuze kuhusu kazi yako unayoifanya na je vitabuvinakusaidia nini katika hilo?**
Kazi ninazofanya ni za ofisini kwa Hiyo nipatapo Muda natumia kusoma vitabu. Na inanisaidia katika kufikiria kwa Haraka katika Maisha Yangu ya kila Siku. Kwa sababu najifunza vingi Sana kwenye vitabu

**Ni vitabu gani au vya tanzu ipi unavyopendelea kusoma? Tutafurahi ukitueleza kwa nini?**
Vitabu ninavopenda Zaidi ni Simulizi za kijasusi hasa kamanda Amata.
Kwa sababu vinanifundisha mengi Mimi Kama mwanaume kupambana Mpaka tone la Mwisho ikibidi Hata Kifo ili uweze kufanikiwa katika Maisha

**Wasomaji wengi hutuambia wazi idadi ya vitabu ambavyo wamesoma kila mwisho wa mwaka… Labda nawe wawea tueleza, kwa mwakaulopita umesoma vitabu vingapi?**
In short nimesoma vitabu vingi kwa Mwaka. Ila Kusema idadi inanipasa nikae nianze kujumlisha ila nimejitahidi nimesoma vingi, tena vinginevyo ninarudia kusoma.

**Unaweza kutueleza mbinu unazotumia katika kufanikisha zoezi la usomaji vitabu?**
Mbinu ninazotumia ni kwa kutumia computer au Simu hasa nikiwa nimelala Mpaka usingizi unanipitia nikiwa nimeshika Simu. Au computer nipatapo muda mchana natumia kusoma vitabu ninavopenda

**Unawaambia nini wale wasiopenda kusoma vitabu?**
Wale wasiopenda kusoma vitabu nawaalikeni muanze kusoma vitabu kwani vinaburudisha na kusoma matukio kama ya ukweli na miji au nchi zinazotumika kama Kishasa, Dar es Salaam, Urusi, Brazzaville, Tanzania, USA, South Africa, Malawi, Congo, Uingereza , ujerumani, Madagascar, Mali, n.k

Naomba tusome vitabu kwa afya zetu kwani vinaondoa Mawazo *negative* katika mioyo yetu.

Nashukuru Sana kamanda Amata kwa Kalamu Yako. Tusonge mbele.



**Sebastian Mapunda**

**KUSOMA NI KUZALIWA UPYA!**

# 2080



**2080**
**LAZIMA IWEZEKANE!**
**Miaka na mikaka, mwanadamu amekuwa katika utafiti mkubwa wa kutakaaweze kuishi katika mwezi au hata sayari yaMars. Lakini isivyo Bahati, kila jaribio lilionekana kukumbwa na vikwazo vingisana.**
**Mwaka 2080, mwanasayansi Mwafrika, Justus Mokael anajaribu tena.**

**Je atafanikiwa?**

**- 01 -**
**Katikati ya Jangwa la Sahara**
**Mwaka 2080**

Katikati ya vumbi la Jangwa la Sahara, ambako mchanga huimba wimbo wa joto nyakati za mchana, kulisimama himaya ya kisayansi—Saharan Space Agency. Hapa, Justus Mokaeli, jabali la sayansi ya anga, alikuwa amezama katika vilindi vya fikra.

Macho yake hayakuwa yakitazama kuta za maabara, bali yalikuwa yakitazama mbali, kuvuka anga la buluu, kuelekea kwenye weusi wa milele wa ulimwengu.
Mbele yake palikuwa na TSD *(Transparent Soft Display),* kioo chepesi kama hariri ya dharura lakini chenye uwezo wa kupakata data za galaksi nzima. Justus hakuhitaji kugusa kioo hicho kwa vidole vyake vyenye makovu ya utafiti; badala yake, aliunganishwa na ulimwengu wa kidijitali kupitia *AI Chip* iliyopandikizwa mwilini mwake. Mawazo yake yalisafiri kama umeme, yakitiririka kutoka kwenye niuroni za ubongo wake hadi kwenye mfumo mkuu wa kompyuta.
Kila dukuduku lililomsumbua, kila swali lililochipuka akilini mwake, lilijitokeza papo hapo kwenye kioo hicho kwa amri ya mfumo wake wa fahamu.

Kwa muda mrefu, Mokaeli alikuwa akifukuzana na mzimu wa ndoto ya kale: maisha ya mwanadamu katika sayari ya Mars na Mwezini. Alikuwa akichambua kumbukumbu za miaka hamsini na nne iliyopita—zama ambazo wanasayansi walikuwa kama watoto wanaojifunza kutambaa gizani. Walikuwa na nadharia, walikuwa na hamu, lakini walikosa ufunguo wa kiteknolojia aliokuwa nao sasa.

"Lazima tufike kilele ambacho wazee wetu walikiona kwa mbali," Justus alinong'ona, sauti yake ikisikika kama mwangwi ndani ya chumba hicho kitupu. Alisimama, mwili wake ukijawa na msisimko wa kigunduzi. Mtu mmoja alimuwaza akilini mwake.
Ghafla, hewa ya mule ndani ilijawa mwanga wa rangi ya zambarau. Mwanga ule ulianza kujisuka katikati ya chumba, na sura ya mwanamke mrembo chotara ilionekana, alikuwa Stacy—mshirika wake mkuu kutoka Marekani— sura ile ikatokea kupitia teknolojia ya hologram. Stacy hakuwa hapo kimwili, lakini kupitia *Electro-think*, kila hisia na wazo la Justus lilimvuta Stacy kuingia kwenye faragha yake ya kiakili.

Katika karne hii, simu za mkononi zilikuwa zimezikwa katika kaburi la historia; sasa, binadamu waliongea kwa kutumia lugha ya fikra.
"Justus, nimehisi mawimbi ya mawazo yako tangu asubuhi. Unataka tufanye kazi pamoja?" Stacy aliuliza, sura yake ya hologramu ikionyesha tabasamu lenye matumaini lakini lenye chembe za hofu.
"Stacy," Justus alianza kwa sauti nzito, "wazee wetu hawakushindwa kwa sababu walikuwa wajinga. Walishindwa kwa sababu wakati uliwatupa mkono. Mwanadamu Sisi tunao ujana na teknolojia. Mwanadamu hatakiwi kubeba matangi ya hewa. Unajua? Siri ipo ndani ya

miamba ya mwezi wenyewe, yaani Regolith."
Justus alionyesha michoro ya kigiriki kwenye kioo chake. "Asilimia 45 ya miamba ya mwezi ni oksijeni iliyojificha. Tunahitaji kuikomboa hewa hiyo ili mwanadamu apumue bila kifungo cha mashine awapo mwezini."
Sasa haikuwa surapekee ya Stacy, bali alionekana wote kana kwamba kasimama mbele ya Justus. Stacy alipiga hatua kuelekea kwa Justus, pindo za vazi lake la kidijitali zikimetameta kama unga wa almasi.
"Lakini kuna vikwazo, Justus. Kani ya chini ya uvutano itawafanya binadamu wawe kama manyoya. Na vipi kuhusu mionzi ya ulimwengu? Labda tusiwapeleke binadamu wa kawaida, labda tuumbe binadamu wapya kimaabara, viumbe wasiohitaji oksijeni."

Wazo hilo lilimfanya Justus atulize mboni zake. "Kuumba binadamu kwenye chupa? Hiyo ni hatua kubwa, Stacy. Lakini mimi bado ninaamini katika asili. Nataka mwanadamu akanyage vumbi la mwezi bila suti nzito ya anga. Nataka ahisi ubaridi wa miamba ile kama anavyohisi upepo wa Sahara."

**- 02 -**
**Safari ya SFS-5**

Miezi kumi na moja ya maandalizi makali ilifuata. Kila sekunde ilikuwa ni mapambano kati ya akili na asili. Mokaeli, Stacy, na timu ya wataalamu walijiandaa kwa safari iliyopewa jina la 'YoYa, yaani Yote Yawezekana'.
Waliondoka duniani kwa kutumia SFS-5 (Space Fastest Shuttle), chombo kilichokuwa na kasi ya ajabu, kikisukumwa na nishati ya *antimatter*. Safari ya kuelekea mwezini, ambayo zamani ilichukua siku kadhaa, sasa ilimalizika kwa saa kumi na tano tu—muda mchache kuliko safari ya basi kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza.
*****
Wakiwa mwezini, kazi nzito ilifanywa na roboti nane kubwa, kila moja ikiwa na uzito wa kilo mia nane. Uzito huo ulikuwa muhimu ili kuziimarisha dhidi ya kani ndogo ya uvutano. Kwa kutumia miale ya Laser, roboti hizo zilipasua miamba na kukusanya tani za *regolith*, zikizitayarisha kwa ajili ya majaribio makuu duniani.

Waliporejea duniani, majaribio yalihamishiwa kwenye maabara ya siri iliyojengwa kilomita kadhaa chini ya mchanga wa Sahara. Hapo kulikuwa na mtambo wa LOER *(Lunar Oxygen Extraction Reactor)*, uwanja mkubwa wa vioo na vyuma vilivyopangwa kwa teknolojia ya hali ya juu.

"Hapa ndipo tutapoandika historia," Justus alisema, macho yake yakionyesha asilimia 52 ya mafanikio ya uzalishaji hewa.
Lakini, kama wasemavyo wahenga, maji yakijaa humwagika. Wakati ndoto ilipokaribia kuwa kweli, kosa moja la kimitambo, pengine ni shinikizo lililozidi uwezo wa vioo vile, lilisababisha kishindo kilichotikisa misingi ya jangwa.

Maabara yote ilipasuka. Milio ya vyuma vinavyopasuka na kioo kinachosambaratika iliziba masikio.
Kazi ya miaka, jasho la maelfu ya wataalamu, na matumaini ya mabilioni ya watu, yote yalisambaratika na kuwa vumbi. Katikati ya moshi na giza, Justus Mokaeli alihisi dunia ikizunguka. Swali moja lilimchoma moyoni: *Je, mwanadamu ni mgeni katika ulimwengu huu, au ni mfungwa wa kudumu wa dunia?*
Nguvu zilimuishia. Alihisi magoti yake yakilegea, na giza nene likamfunika huku akianguka kwenye sakafu ya maabara yake iliyobomoka.

*Mwisho wa kipandecha kwanza!*

# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—11

**MTUNZI: ASHA SIRAJ**
**Whatsapp 0789044345**



**UTANGULIZI**

**Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhila**

***Ilipoishia…***

Baada ya kumaliza kupata kifungua kinywa nilipumzika kidogo kisha nikaanza kuandaa chakula cha mchana, dokta alikuwa anatoka kazini jioni majira ya saa kumi na moja alipenda sana kula chakula cha nyumbani.

Siku zilizidi kusonga mbele na miezi ikapita nikiwa pale kwa dokta, nilimuomba dokta ikiwezekana yule binti asije tena naweza kufanya usafi mimi kama mimi, labda siku za *weekend* hivyo anaweza kuja kunisaidia ila kwa siku hizi nyingine aache nifanye mimi.

Nilipenda sana usafi hivyo sikuruhusu mazingira yawe machafu kila siku dokta alipokuja nyumba alihakikisha anakuja na zawadi ya chocolate maana nilikuwa napenda sana kula chocolate.

Ukaribu wetu ulizidi kuwa mkubwa dokta hakutaka niende mbali na yeye alipenda sana kula chakula changu, hakutaka tena kupikiwa na mtu yeyote zaidi yangu.

Ule ukaribu ulitupelekea mpaka kujenga mahusiano mimi pamoja na dokta, mimi ni nani hadi nimkatae amekuwa kaka angu au ndugu yangu, mapenzi yetu yalizidi kushamiri huku nikisubilia matokeo yangu yatoke.

Matokea yangu yalitoka nilifaulu vizuri, hivyo alinimbia niende chuo na wala sio mambo ya kuendelea na kidato cha tano.

Alikuwa ananipeleka chuo asubuhi akiwa anaenda kazini na jioni alinipitia tuondoke wote nyumbani. Mapenzi yetu yalizidi kushamiri.

Siku ambayo sintokaa nikasahau kwenye maisha yangu mpaka pale nilipopelekea kumchukia sana dokta Shahdu ni pale nilipogundua ana mahusiano na mwanamke mwingine. Hakika nilijikuta najutia kuwa nayeye.

Baada ya miezi sita mimi na dokta Shahdu tukiwa kwenye penzi jipya, majira ya saa mbili usiku dokta Shahdu akiwa *washroom* simu yake aliiacha mezani.

Gafla ilianza kuita. Kwakuwa mimi nilikuwa mpenzi wake ilinibidi niende kuangalia ni nani aliyekuwa anampigia, ila moyo wangu ulisita.

Niliamua kuachana na ile simu na kuwa busy na mambo yangu kipindi hicho tayari nilikuwa na simu yangu. Simu iliendelea kuita kwa mara nyingine, nilinyanyuka na kwenda kuipokea jina tu lilinifanya nichanganyikiwa pale .

Haloo nilipokea! Sauti nyororo ilifika kwenye ngome ya masikio yangu, *"baby uko wapi? Maana nakupigia simu hupokei kuna tatizo my wangu?"*

Kiwewe nilichokuwa nacho kilisababisha simu inidondoke chini kutoka kwenye mikono yangu, wakati huo dokta wangu alikuwa amemaliza kuoga amekuja kuketi namimi ukumbini.

Nilibaki nimemtumbulia macho nilitamani kumrukia walau nimmeze wenda zile hasira nilizokuwa nazo zote zikaisha.

Kiufupi nilishindwa cha kufanya zaidi ya kubaki mdomo wazi tu huku machozi yakinitiririka sijui kama huyo binti alikata simu au la

Me sikujali kuhusu yeye, nilinyanyuka kuelelea chumbani kwangu huku nikilia kama mtu aliyepigwa vile. Kumbe siku zote dokta wangu alikuwa ananiongopea, hakuwa na mapenzi ya dhati kwangu.

Alinifuata kwa nyuma akiwa ananiuliza kama nina shida. *Hivi huyu mwanaume ni zombi nyie eti ananiuliza nina shida ? Wakati amenikuta kabisa nina simu yake!* Nilijiwazia.

Niliingia chumbani nikajaribu kuufunga mlango wangu. Kwa muda huo sikutaka kusumbuliwa kabisa, nilisukuma mlango kwa nguvu nikijaribu kuufunga ila yeye hakuwa tayari, alisukuma mlango kwa nguvu hadi nikaishiwa nguvu

# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—11

za kuufunga na ufunguo.
"Shahdu sihitaji kuiona sura yako mwanaume asiyekuwa na haya wewe, unanidanganya unanipenda kumbe una *vishikwambe* vyako huko,
Jaribu kunionea huruma mimi ni binadamu hivyo, huwazi kabisa kuhusu mimi unachokiwaza wewe ni kuipoteza furaha yangu tu na wala huna nia njema na mimi. Yani una mwanamke mwingine kisha ukija kwangu unaishia kunitumia tu nakuniongopea unanipenda," nililalama huku chozi mpaka kifuani.

Siku hiyo haikuwa siku nzuri kwangu, Shahdu alijaribu kunibembeleza Kadiri ya uwezo wake, ila mimi sikuwa tayari kumsikiliza kwa sababu nilimuona muongo na mlaghai .
Aliniomba kunitoa *out* siku hiyo ila mimi sikuwa tayari nilihisi kabisa ananipigia kelele tu, nilimuomba sana anipishe na kila mmoja afanye mambo yake .
Baada ya kumwambia hivyo aliondoka kabisa nakuniacha chumbani peke yangu, nililia sana sikuwa na rafiki walau hata wa kumwambia shida zangu uenda angenielewa

Asubuhi yake kulikucha, siku hiyo sikutaka hata anipeleke chuo, kila mmoja aliondoka kivyake mimi nilipanda kwenye bajaji na kuodoka zangu.
Ilipita wiki nzima ndani bila kuongeleshana, nilifanya majukumu yangu mle ndani nilikuwa napika anakula na kulala kila mmoja alijiweka *busy* namabo yake,
Me nilipigania usiku kucha kwa kusoma maana nilihisi kabisa hata mapenzi ni uwongo mtupu, kabla mambo hajawa mabaya nipambanie kusoma tu.


Siku mmoja majira ya saa kumi na mbili nikiwa ndani naangalia tivii mara mlango ulisukumwa, alikuwa dokta akiwa amelewa. Pembeni yake alikuwa ameshikiliwa na mdada ambaye sura yake ilikuwa ngeni kwangu.
Nilisimama wima nikijiuliza zarau gani hizi hadi naletewa mwanamke ndani.
"Shahdu umeona haitoshi ukaamua kuja na malaya wako humu ndani, kama umenichoka unaweza kusema tu ," nikamwambia bila kuogopa.

Nilijiweka sawa na kumsogelea huyo mwanamke, nikiwa najaribu kumuachisha Shahdu kwenye mikono ya mwanahizaya huyo.
"Kaa mbali na mwanamke wangu wewe... kama umechoka unaweza kuondoka humu ndani sikukuleta hapa mimi!" Shahdu alinifokea. Harufu ya pombe ndio ilitapakaa kinywani mwa Shahdu
"Umesikia wewe *mburula*, *baby* wangu kasema kama umechoka ondoka wacha sie tumuhudumie," yule mwanamke akaongea kwa dharau.
Yani kwa hasira nilijikuta namzaba kibao yule mwanamke maana niliona anataka kunipanda kichwani.
"Eti *mburula* kahaba wewe!" nikamwambiakwa hasira.
"*Baby* unaona huyo kinyago wako ananipiga?" aliongea mwanamke huyo.
"*Baby* achana naye!" Shahdu akajibu. Haoooo! Waliongozana mpaka chumbani. Yani nilihisi haja kubwa ghafla, kizunguzungu sio kizunguzungu, sijui kilikuwa *kichinachina* mwenzenu sikuwa naelewa kabisa kinachotokea.
Nililia sana usiku huo, akufukuzae kweli akwambii undoka, mambo hayo yalidhidi kuendelea kila siku ilfika mda sasa nikachoka, nilitamani kuondoka ila nikiangalia sikuwa na pa Kwenda; kwa shangazi ndo kama vile, mwenzenu nilihisi uchizi ghafla.

*Kazi sina wapi niende mimi?* Niliwaza.. Au ndiyo sababu Shahdu anafanya hivyo, maana anajua sina pa kwenda anaamua kunikomoa kwa staili hiyo.
Nilikonda mithili ya mgonjwa wa ukimwi sikuwa na furaha ndani ya jumba hilo, nilijihisi myonge kila wakati kutokana na tabia alizokuwa akizionyesha Shahdu ndani ya jengo hilo.

Ilifika muda akawa ananiambia mimi nitaendelea kuwa mfanya kazi ndani ya nyumba hiyo, nashukuru hakuwahi kunizuia nisiende chuo, yote alikuwa anafanya ila kwenye swala la ada alilipa vyema.
Yani sikuwa namuelewa kabisa kwanini ananaifanyia mambo kama haya, kama nimakosa yalikuwa ya kwake mwenye sasa kwanini ananiadhibu mimi.

***Itaendelea...***



## SAFARI YA KWANZA YA SINBAD

Tambua kuwa baba yangu alikuwa ni mfanya biashara mkubwa sana katika nchi ya baghdad wakati wa utawala wa sultan harun Rashid. Baba yangu alifariki miaka 21 iliyopita nilipokuwa kijana kama wewe. Wakati huo nilikuwa na marafiki wengi sana. Na nilianza kutumia mali aloniachia baba na hatimaye akakaribia kuisha na marafiki wakanikimbia. Na hapo ndipo nilipoamua kuanza biashara za majini, yaani kuuza bidhaa sehemu mbalimbali za visiwa.

Nilijiandaa vizuri kwa ajili ya safari yangu ya kwanza. Na maandaliizi yalipokuwa tayari tulianza safari ya kubiashara. Safari ilikuwa salama kabisa kwa muda wa masiku. Tulipita visiwa kadhaa tukiuza na kununua. Kwa upande wangu biashara haikuwa mbaya ijapokuwa ugeni ulinisumbuwa sana. Kwa ujumla nilifurahia safari ile. Baada ya kutembea visiwa kadhaa tuliamua kumalizia katika viziwa vingine ili tuweze kurudi nyumbani. Ilitikea sikumoja ghafla upepo ulianza kubadilika na jahazi likashindika na kudhibitiwa na manahodha.

Upepo ulizidi mpaka nahodha akaamua kukiachia chombo kiende kokote, hali iliendelea kuwa mbaya mpaka bidhaa zikaanza kutumbukizwa majini ilikuokoa ualama wa maisha. Haliiliendelea kuwa mbaya hata chombo kikaanza kunywa maji. Watu wakaanza kuania rohozao, na kuanza kushika mbao zilizovunjika kutoka kwenye jahazi. Mimi nilipata mbao moja na ilinipeleka mbali zaidi ambapo sikuweza kuona hali za wenzangu kilicho endelea.

Kwa upande wangu mawimbi ya maji yalinipeleka mbali sana, nikiwa nimeshikilia tawi lile hata sikusubutu kuliachilia. Nilipofika hali ambapo sijielewi kwa kuchoka ghafla nikaona kunaweupe mbele yangu, kuangalia vizuri kilikuwa ni kijisiwa kidogo. Basi nikajitahidi kujizuia huku nikawa naiba maji ili yanipeleke kule. Kwa bahati njema kaupepo kakanipeleka kwenye kisiwa kile. Kwa msaada wa mizizi ya miti niliweza kutoka kwenye maji yale.

### KISIWA CHA UOKOZI

Nikajisogeza vyema hata nikafika kwenye kivuli. Na kwa kuwa miguu yangu haikuwa na nguvu nilibuluzika tu. Nililala bila ya kijitambua niliamshwa na maji yaliyokuwa yakinipiga miguuni kumbe maji yalikuwa yanajaa. Haukupita muda ghafla nikaona kuna kijahazi kinaingia kikiwa kina mifugo kadhaa. Walipofika pale kisiwani wakawafungulia mifugo yao na kuanza kuwaosha na kuwapaka dawa. Mmoja wao akaenda mbali kidogo akaja na majani mengi sana na kuanza kuchagua baadhi ya ng'ombe na kuanza kuwapa majani yale.

Niliwafuata na kuwaomba msaada wa chakula. Wakanipa maziwa na mkate wa nyama. Nilipomaliza kula wakaniuliza habari yangu na eneo lile na nikawaeleza kila kitu. Basi wakaniambia kama ungekuja kesho usingetukuta na pengine ungefia hapa maana hakuna majahazi yanayokuja hapa ila ni sisi tu na huchukuwa miezi 3 ndo tunakuja tena. Na kisiwa hiki hakina chakula, hivyo pengine ungeishia kufariki hapa. Basi wakanipatia na nguo na nikawauliza pia sababa ya wao kuja hapa na ni kinanani wao.
Mkubwa wao akanieleza kuwa wao ni watumishi wa mfalme aliyepo karibu na eneo hili. Mfalme huyo amekiteua kisiwa hiki kama eneo la kutibia mifugo yake na amepanda majani maalumu kama dawa ya mifugo yake. Hivyo eneo hili hawaruhusiwi watu wengine hapa. Basi walipomaliza shuhuli zao walifunganya mizigo yao na kuchukuwa majani mengi na nikaondoka pamoja nao.

Tulipofika kwenye utawala wao wakanipeleka kwa mfalme wao na nikamueleza mimi ni nani na nini kazi yangu na kumueleza kuwa natokea baghdada nchini kwa sultan Harun Rashid. Basi mfalme yule nikamueleza mengi kadir alivyouliza na mimi sikuwacha kuu;liza mambo kadhaa. Kwa haraka zaidi mfalme yule alionekana kunipenda sanan na kunikubali. Basi alinifanya katika watu wa karibu yake na ni kama mshauri pia. Niliishi pale nikawa nafanya biashara chini ya mfalme yaani nilikuwa naendeleza bishara za mtoto wake wa kike.

*Itaendelea toleo lijalo*

**Je unafurahishwa na jarida letu?**

**Tuambie kupitia Whatsapp**

**+255 766 974 865**


TUZO YA KISWAHILI
YA SAFAL YA FASIHI
YA AFRIKA
10 YEARS OF
LITERATURE
Submit your manuscript for a chance to shine in the Safal Kiswahili Prize for African Literature 2025
AWARD CATEGORIES AND PRIZES:
1st Prize for Fiction: $5,000 USD
2nd Prize for Fiction: $2,500 USD
(Manuscript must contain a total word count between 40,000 and 60,000)
1st Prize for Poetry: $5,000 USD
2nd Prize for Poetry: $2,500 USD
Poetry manuscripts with not less than 60 pages
1st Prize for Short Stories: $2,500 USD
The total word count should be 40,000 (each individual story must be between 1,000 & 6,000 words)
Submit your manuscript and join us in celebrating the richness of Kiswahili literature.
Please send your submissions to:
kiswahiliprize@kiswahiliprize.org
OR
Visit our website for more information and submission guidelines:
www.kiswahiliprize.org
Submission Deadline:
March 31st, 2026
SAFAL GROUP
ALAF
MRM
MABATI ROLLING MILLS

# NAGUIB MAHFOUZ: Wasifu wa Mtaa Uliogeuka Kuwa Ulimwengu

**Na: Mervat Sakr**


Naguib Mahfouz amezaliwa Disemba 11, 1911 katika mtaa wa kihistoria wa Al-Gamaliya, ambako misingi ya awali ya utoto wake iliundwa. Baadaye, safari ya maisha yake ilienea kati ya Al-Abbasiya, Al-Hussein na Al-Ghouriya; mitaa ya kale ya Kairo ambayo haikuwa tu vituo vya makazi, bali iligeuka kuwa kitambaa hai katika kazi zake za fasihi, na jukwaa pana la kibinadamu lililoakisi mtazamo wake kuhusu ulimwengu.

Mahfouz alimaliza elimu yake ya msingi katika umri mdogo, kisha akaingia Chuo Kikuu cha Kairo mnamo mwaka 1930, na kuhitimu katika Idara ya Falsafa mnamo mwaka 1934 akipata shahada ya kwanza ya sanaa. Jina lake la kipekee lilikuwa na maana ya kibinadamu, kwani baba yake alimpa jina hilo kwa heshima ya daktari mashuhuri Naguib Pasha Mahfouz aliyesimamia kuzaliwa kwake kwa taabu.

Tangu miaka ya 1940, Naguib Mahfouz alianza mradi wake mkubwa wa fasihi, mradi uliodumu kwa zaidi ya miongo sita, ambapo aliandika riwaya, hadithi fupi na maandishi ya filamu. Hakuwahi kuhama Misri, kwani ndiyo iliyomfunulia ulimwengu. Katika riwaya zake, "mtaa" uligeuka kuwa kioo cha ulimwengu mzima, ukifupisha migogoro ya kibinadamu, kufichua mabadiliko ya jamii, pamoja na mahangaiko, ndoto na kuvunjika kwa matumaini ya tabaka la kati.

Katika taaluma yake ya kazi, Mahfouz alishika nyadhifa kadhaa muhimu za kiutamaduni na kiutawala; kuanzia kuwa mwandishi katika usimamizi wa chuo kikuu, hadi katibu wa bunge, kisha mkurugenzi wa udhibiti wa kazi za kisanii, rais wa Taasisi ya Filamu, na mshauri wa Waziri wa Utamaduni katika masuala ya filamu. Alikuwa mshiriki hai katika taswira ya kitamaduni ya Misri, akiwa mwanachama wa Baraza Kuu la Utamaduni, Klabu ya Hadithi na Chama cha Waandishi.

Safari yake ya kifasihi ilianza kwa kuandika hadithi fupi mnamo mwaka 1936, kisha akaelekea kwenye riwaya za kihistoria zilizochota kutoka Misri ya kale, kabla ya kutulia katika riwaya za kijamii. Alifikia kilele cha ukomavu wake wa ubunifu kupitia trilojia yake maarufu: Bayna Al-Qasrayn (Kati ya Majumba Mawili), Qasr Al-Shawq (Jumba la Shauku), na Al-Sukkariyya (Sukariyya), aliyoiandika mnamo mwaka 1952, ingawa haikuchapishwa kikamilifu hadi



mwaka 1956. Baadaye, kazi zake zilichukua mwelekeo wa kifalsafa na wa alama, kama ilivyo katika Awlad Haratina (Watoto wa Mtaa Wetu), Al-Harafish, na Rihlat Ibn Fattouma (Safari ya Ibn Fattouma).

Kati ya mwaka 1952 na 1959 aliandika idadi kubwa ya miswada ya filamu, huku riwaya zake baadaye zikigeuzwa kuwa kazi mashuhuri katika skrini kubwa na ndogo, kama Bidaya wa Nihaya (Mwanzo na Mwisho), Al-Liss wa Al-Kilab (Mwizi na Mbwa), na Tharthara Fawq Al-Nil (Mazungumzo Juu ya Nile), hali iliyomfanya kuwa mwandishi wa Kiarabu ambaye kazi zake nyingi zaidi zimegeuzwa kuwa filamu na tamthilia.

Naguib Mahfouz aliacha zaidi ya kazi hamsini za fasihi, zilizotafsiriwa katika lugha 33, na kazi zake zikasajiliwa katika Maktaba ya Congress ya Marekani. Ulimwengu uliandika kumhusu kwa lugha mbalimbali, kama utambuzi wa nafasi yake kama mmoja wa nguzo za fasihi ya kibinadamu.

*Inaendelea ukurasa wa 27...*


## MY LIFE, MY PURPOSE – 03

UCHAMBUZI WA KITABU CHA RAIS MSTAAFU BENJAMIN MKAPA

**"MY LIFE, MY PURPOSE"**

**Na PROF. RWEKAZA MUKANDALA**

**{Imetolewa kutoka mtandaoni}**




**3. MAISHA NA KAZI**

*Inaendelea…*

Alirudi na kuanza kazi chini ya Mwalimu kama Mhariri Mkuu, Mhe. Mkapa alikuwepo Arusha wakati wa Azimio mwenzie Nsa Kaisi ndiye aliyebuni neno la Arusha Declaration, walilitumia kwenye The Nationalist, Mwalimu akalipenda, basi hayo maamuzi yakaitwa hivyo.

Mhe. Mkapa aliruhusiwa kuhudhuria mikutano ya kamati kuu ya TANU, ambayo wakati ule ilitawaliwa na malumbano ya hoja na uchambuzi yakinifu ambao umepotea. Alihusika katika kutayarisha sera mbalimbali za chama kutokana na umahiri wake wa kumudu lugha.

Mwalimu na msaidizi wake Joan Wicken ndio walio mfundisha ujamaa na alivutiwa na msimamo wa usawa na umuhimu wa kujitegemea. Aliunga mkono wazo la Jeshi la Kujenga Taifa na akamuomba Mwalimu akamkubalia ajiunge kwa hiari. Alijiunga na kuhitimu. Siku ya kuhitimu Mwalimu alikuwa ndie mgeni rasmi. Mheshimiwa Mkapa alichaguliwa na wenzie kusoma risala na Mwalimu alicheka sana alivyomtambua kuwa ni yeye kwani alikuwa amepoteza ratili nyingi za uzito. Alikuwa slim fit. Mheshimiwa Mkapa aliitwa huko "The Clinic" Msasani mara kadhaa.

April 1972 Mwalimu alimteua kuwa Mhariri Mtendaji wa Daily NewsMuda mfupi baadaye Mwalimu alimteua kuwa Press Secretary wa Rais. Anasema huu ndio ulikuwa mwanzo wa maisha yake kama mwanasiasa.Mwaka huohuo, Mwalimu alimuagiza aanzishe Shirika la Habari Tanzania – SHIHATA na kuwa Mtendaji Mkuu wake.Mwaka 1976 akamteua Balozi huko NigeriaMwaka mmoja baadaye akaitwa tena " The Clinic" na kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. Hapa alikuwa kama msaidizi wa Rais kwani Mwalimu ndiye aliyeendesha mambo ya Nchi za Nje. Alifanywa pia Mbunge wa kuteuliwa .Aliteuliwa kuwa Balozi wa Canada 1982Balozi Marekani 1983 – 1984Akateuliwa waziri wa habari na utamaduni 1980 – 1982Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje tena 1984. Anabaini kuwa kwa kweli Mwalimu aliipa familia mtihani mkubwa na hii hamahama, lakini familia chini ya mama Anna walikubali na kupokea yote kwa mikono miwili

Hakika Mwalimu ndiye shujaa mkuu wa simulizi hii. Mheshimiwa Mkapa anamueleza Mwalimu kuwa:

Alikuwa jasiri, na kiongozi lazima awe jasiriAlikuwa msikivu, kamwe hakumkatiza mtu hata kama alikuwa anaeleza pumba tu.Alikuwa mtu wa msimamo, hakuyumbayumbaAlikuwa mpatanishi na mjenga madaraja kuwaunganisha mahasimu.Alikuwa communicater wa ajabuAlikuwa fundi wa kutafuta sehemu za makubaliano kati ya wanao tofautianaAlikuwa mtaalamu wa kutumia mawazo ya wengine kurutubisha na kuboresha ya kwakeAliupa umuhimu wa kipekee Umoja wa KitaifaHakupenda ukandamizaji ndio sababu hakupenda kuikalia Uganda baada ya vita 1980

Mheshimiwa Mkapa anasema "Mwalimu alikuwa mwalimu wangu kwa kila kitu".

Alikuwa mwana demokrasia mtu aliyempenda kama mrithi wake mwaka 1985 alipokataliwa na wenzie katika kamati Kuu, Mwalimu alikubali.Alikuwa kiongozi mwenye maono – visionary, alingalia maslahi na mustakabali wa Taifa ndani na nje ya mipaka yake.

Wazazi wa Mheshimiwa Mkapa walifariki akiwa Waziri, wakiwa na furaha na faraja kwa mafanikio yake, ingawa hakuwa Padre, Daktari au Mwalimu kama baba yake mzazi mzee Matwani alivyotaka.

***Itaendelea...***


# HABARI PICHA




Wanafasihi nguli waliohudhuria kongamano la KAKAMA huko Zanzibar. Mwenye Blauzi Nyekundu ni Eva Mrema Mwenyekiti wa CHAFAMA



Katika moja na mbili za kukuza lugha ya Kiswahili duniani, pichani ni Corona Cermak mwandishi wa hadithi za Watoto akionesha utamaduni wa Mswahili huko Australia.




Cde Anna Mbise akipokeazawadi ya kitabu cha MTAFITI kutoka kwa mwandihi nguli Hussein Issa Tuwa



Mwandishi wa KOVU LA MOYO na MAZUNGUMZO YA WANAWAKE Bi. Mariam Mbano akiwa mapumzikoni jijini Dubai. Waandishi tembeeni mjifunze...

**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

## KAMA MOSHI

Usilinge ndugu yangu
Hata kukufuru Mungu
Pabichi pako pakavu pangu
Uzima hajatupa Mzungu.

Kama moshi tapea
Kwa upepo tapotea
Mbingu zitatupokea
Mawnguni 'potelea

Kama moshi taondoka
Angani tasambaratika
Maisha tatamatika
Kama Mola atavotaka

Kama moshi iweni
Kwa kutokea motoni
Toka katika dohani
Panda mpaka angani

Kama moshi sifuni
Wingu, jua na nyuni
Pamoja shikamaneni
Mwenyezi mtukuzeni

Kama moshi we ishi
Uzima kamwe hauishi
Duniani milele hutoishi
Bali kwa Muumba Taishi

Kama moshi geuka
Umbolo badilika
Uwe tititi hakika
Kiumbe usiyeeleweka

Mja, ishi kama moshi!

**Shujaa Maneno**
**Bagamoyo Pwani**

## FURAHA

Furaha toka moyoni
Yatuweka furahani
Yaificha kimyani
Inayottesa huzuni

Furaha ilo usoni
Ndo itokayo moyoni
Yatutakasa mwilini
Na Kutenda kwa makini

Furaha ni kituchema
Kinachotfanya twahema
Kwetu hakuna mahema
Wala asiye rehema

Si kinababa si kinamama
Kwetu kede ni wema
Furaha tunayoisema
Ndo hiyo tunanema

Bubujiko la furaha
Latweka mbali na karaha
Daima siye tuna raha
Kabila yetu furaha

Cheka bwana acha unaa
Kipi chakupa kinyaa
We cheka kila saa
Hakuna wa kukuona kichaa

Kucheka ndiyo dawa
Tangu Adamu na Hawa
We mbona wachachawa
Waogopa lako bawa

Cheka bwana, nononono unamnunia nani?

Shujaa Maneno!

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**

# TANGAZO


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI
KASHMIR
OPERESHENI
KASHMIR
Sasa Kinapatikana
kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE
NAKALA YAKO
DAR ES SALAAM
Duka la Kona ya
Riwaya
Kinondoni Morocco
Simu:
0655428085
Zammira


KAMANDA AMATA
MSALITI
"Kamwe hatoki upande wa adui yako"
MSALITI
15,000/=
Kona ya Riwaya
BOOKSHOP
Fika dukani kwetu au
wasiliana nasi Kwa
Simu
0655 428 085
Mliopo mikoani
tunakutumieni.


KINAPATIKANA
ARUSHA
Kinapatikana Kwa Ally Said Shaban, nje
tu ya KIMAHAMA Bookshop
Simu: 0757690302 na 0656744390
KAMANDA AMATA
MSALITI
"Kamwe hatoki upande wa adui yako"
15,000/=
tu
Jipatie Nakala
Yako Sasa!


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI
KASHMIR
OPERESHENI
KASHMIR
Sasa Kinapatikana
kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE
NAKALA YAKO
ARUSHA
Nje ya Duka
KIMAHAMA
Simu
+255 757 690 302
ALLY SAID

# KUTOKA MAKTABA
## Hammie Rajab

Hammie Rajab alikuwa mwandishi maarufu wa vitabu vya riwaya na fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania, na pia muongozaji wa filamu. Alikuwa mmoja wa waandishi wakubwa wa vizazi vya miaka ya 1970–1980 ambao kazi zao zimekuwa na athari kubwa kwenye fasihi ya Tanzania.

**Vitabu na kazi zake**

Hammie Rajab aliandika vitabu mbalimbali vinavyojulikana, vingi vikiwa katika lugha ya Kiswahili, na vinavyotumika pia kama nyenzo za elimu au burudani. Baadhi ya vitabu vyake ni pamoja na:

**Ufunguo wa Bandia** (riwaya ya Kiswahili, ilichapishwa mara ya kwanza 1979).
**Miujiza ya Mlima Kolelo** (Hadithi iliyo chapishwa 1982).
**Sanda ya Jambazi** (riwaya, ilichapishwa 1999).
**Roho Mkononi** (riwaya ya Kiswahili).
**Ama Zao – Ama Zangu** (riwaya ya Kiswahili).
**Somo Kaniponza**
**Gubu la**
**Wifi**
**Najuta Kuolewa**
**Simu ya Kifo**
**Rest in Peace**
**Dear Mother**

Pamoja na hizo, zipo kazi nyingine nyingi.

**Mchango wake**
Hammie Rajab alikuwa mmoja wa waandishi wakubwa wa fasihi ya Kiswahili na kazi zake ziliitwa *"classic"* ndani ya fasihi ya Tanzania. Kazi zake hazikuishia tu kwenye vitabu bali zingine zilitumiwa pia kufanywa filamu.
Yeye alichangia katika kukuza fasihi ya Kiswahili na kutengeneza kazi ambazo zimekuwa zikisomwa kwa miaka mingi baada ya kuchapishwa.

**Hammie Rajab ni nani hasa?**

**Utoto na Elimu**
Alizaliwa mwaka 1936 huko mkoani Morogoro, Tanzania akiwa mtoto wa pili katika familia ya marehemu Rajab Athuman. Jina lake halisi ilikuwa Hamisi Rajab Athuman.

HAMISI RAJAB ATHUMAN (HAMMIE RAJAB)



Alisoma elimu ya msingi katika shule ya Msamvu mjini Morogoro. Baadaye alienda nchini Kenya, ambapo alijiunga na Taasisi ya Mombasa Institute of Muslim Education (MIOME). Huko alisoma kwa miaka mitano na kupata cheti cha taaluma kama fundi makanika.

**Kazi na Uanzishwaji wa Kitaaluma**
Kabla ya kuingia ulimwengu wa uandishi, Hammie alifanya kazi sehemu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kazi za magari na shirika la reli (TRC).

Mwaka 1974 alijiunga na Kampuni ya Filamu ya Tanzania (TFC) kama muongoza filamu. Alipata mafunzo ya filamu na kujiendeleza katika sekta hii, iwe katika uandishi wa vitabu au kuiga kazi zake kwenye filamu.

**✍ Uandishi wa Vitabu**
Hammie Rajab alikuwa mwandishi wa vitabu vya riwaya na hadithi za Kiswahili, na kazi zake zilivutia wengi ndani na nje ya Tanzania.

Kazi zake zilikuwa zikiuzwa na kusomwa sana, ingawa wakati huo soko la vitabu ilikuwa changamoto kutokana na uchumi na utamaduni wa usomaji.

**Filamu na Uandishi wa Script**
Sio tu alitetea uandishi wa vitabu, bali pia alifanya kazi kubwa kuandika na kuongoza filamu. Filamu nyingi alizotengeneza zilikuwa zimetokana na kazi zake za maandishi. Baadhi ya filamu alizoshirikiana au kuziunda ni kama Watoto Wana Haki, Usawa, Benki Yako, Miujiza ya Mlima Kolelo, Gubu la Wifi, Kibuyu na nyingine nyingi.

**Kifo na Urithi**
Alifariki dunia tarehe 21 April 2011 jijini Dar es Salaam akiwa na umri wa miaka 63 na kuzikwa mjini Morogoro.

Kazi yake ya uandishi na filamu imeacha urithi mkubwa wa fasihi na sanaa ya Kiswahili, kuendelea kusomwa na kuifundisha fasihi kwa vizazi vipya.

*Toleo lijalo tutaangazai falsafa ya uandishi wake...*

# ELIMU JAMII

## SAFARI YA MALEZI 8:

**MALEZI KATIKA HATUA TOFAUTI ZA UKUAJI WA MTOTO**

**8.0 Malezi katika Hatua za Ukuaji wa Mtoto**

Malezi bora yanahitaji mzazi au mlezi kuwa na uelewa wa kina wa hatua tofauti za ukuaji wa mtoto, kwa sababu mahitaji ya mtoto hubadilika kadiri anavyokua. Mahitaji haya si kwa upande wa kimwili tu, bali pia kihisia, kisaikolojia, na kijamii. Mtoto hapitii ukuaji wake kwa njia moja tu bali hupitia hatua mbalimbali kadiri miaka inavyoenda.

Kila hatua ina changamoto zake na inahitaji mbinu tofauti za malezi. Ikiwa mzazi au mlezi haelewi tofauti hizi, anaweza kutumia mbinu zisizofaa kwa umri wa mtoto, jambo linaloweza kuathiri tabia, hisia, na maendeleo yake kwa ujumla. Malezi yanayolenga kila hatua husaidia mtoto kukua kwa uwiano, kuendelezwa kulingana na uwezo wake, na kujiandaa vyema kwa changamoto zinazofuata za maisha.

Kwa hiyo, mzazi anapojua tofauti za hatua hizi, anaweza kutumia mbinu zinazofaa kwa kila umri, kuhakikisha mtoto anapata mwongozo unaolingana na hali yake ya ukuaji. Hii inasaidia kumjenga mtoto ambaye ana maadili mema, uelewa wa wajibu, na uwezo wa kukabiliana na changamoto za maisha bila hofu au shaka. Malezi yenye uwiano ni msingi wa kumlea mtoto kuwa mtu mzima mwenye kujiamini, heshima kwa wengine, na mchango chanya katika familia na jamii.

Na. KELVIN JOHN KYARA

0753767930

**8.1 Hatua za Ukuaji wa Mtoto na Malezi Yake**

**8.1.1 Malezi katika Hatua ya Awali (Miaka 0–5)**

Hatua ya awali ni msingi wa ukuaji wa mtoto. Katika kipindi hiki, mtoto hujifunza lugha, kuendeleza uhusiano wa kijamii, na kupata malezi salama na ya karibu sana kutoka kwa wazazi wake. Malezi katika hatua hii yanapaswa kuwa ya karibu, yenye upendo, na ulinzi wa kihisia. Mzazi anapaswa kuwasiliana na mtoto kwa upole na maneno ya faraja, kumlinda dhidi ya hatari, na kuepuka adhabu zisizo na sababu. Nidhamu iwe ya kuelekeza na kufundisha, badala ya vitisho au hasira zisizo za lazima.

Mifano:

i) Mtoto anapotaka kugusa kitu cha hatari, mzazi humzuia kwa upole na kumweleza hatari badala ya kumpiga au kumtishia.

ii) Mtoto anayelia wakati wa kulala, mzazi anaweza kumtuliza kwa kumgusa, kumkumbatia, au kuimba wimbo wa faraja, na si kumlazimisha kwa vitisho vingi.

iii) Wakati mtoto anataka kula mwenyewe lakini anaangusha chakula, mzazi humsaidia kwa uvumilivu na kuonyesha njia sahihi ya kutumia kijiko.

Kila wakati mtoto anapojaribu kutamka maneno mapya au kufanya jambo lolote jipya, mzazi humsikiliza kwa makini, kufuatilia na kumpongeza, akimfundisha thamani ya mawasiliano. Hii humfundisha mtoto mipaka kwa njia chanya na kumjengea msingi wa kujiamini na hisia za usalama.

**8.1.2 Malezi katika Hatua ya Kati (Miaka 6–12)**

Katika hatua hii mara nyingi mtoto huanza kuambatana na jamii, kutoka nje ya familia yake, hususan shuleni. Katika kipindi hiki, mtoto huanza kuelewa sheria, wajibu, na mahusiano ya kijamii. Ni wakati ambapo mtoto hujifunza kutimiza majukumu na kupata uthibitisho wa uwezo wake. Malezi yanapaswa kuhimiza nidhamu, uwajibikaji, na tabia njema. Mzazi anapaswa kushirikiana kwa karibu na walimu ili kufuatilia maendeleo ya mtoto kitaaluma na kitabia. Nidhamu iwe thabiti, yenye haki, na yenye maelezo ya sababu ili mtoto kuelewa kwa nini kanuni au taratibu zinapaswa kufuatwa.

Mifano:

i) Mtoto anapopewa majukumu madogo nyumbani, kama kutandika kitanda , kufanya usafi, humjengea msingi wa uwajibikaji na kujithamini.

ii) Mtoto anayesimamia ratiba zake, kama kuandika majibu ya kazi za shule au kupanga vifaa vya shule, hujifunza kupanga muda na uwajibikaji.

Mzazi anapompongeza mtoto kwa jitihada zake, mfano kujaribu suluhisho la hesabu ngumu, humsaidia kukuza mtazamo chanya wa kujifunza na bidii. Wakati mtoto anauliza “kwa nini lazima nifanye hivi?”, mzazi anatoa



maelezo kwa uvumilivu, akimfundisha kutambua sababu na matokeo ya matendo yake.

**8.1.3 Malezi katika Hatua ya Balehe (Miaka 13–18)**
Balehe ni kipindi cha mabadiliko makubwa ya kimwili, kihisia, na kisaikolojia. Mtoto huanza kujitambua zaidi, kuuliza maswali kuhusu utu wake, na wakati mwingine kupinga mamlaka. Malezi katika hatua hii yanahitaji hekima, subira, na mawasiliano ya wazi. Mzazi anapaswa kumchukulia kijana kama mtu anayekua, kumshirikisha katika maamuzi yanayomhusu, na kumsikiliza kwa makini. Badala ya kutumia amri nyingi, mazungumzo, ushauri, na mwongozo hufaa zaidi.

Mifano:
i) Kijana anaposhirikisha mzazi kuhusu marafiki wake au matatizo shuleni, mabadiliko katika mwili wake nk, mzazi anapaswa kusikiliza, kutoa ushauri, na kuhimiza suluhisho zuri bila kushinikiza.
ii) Kijana anayepanga mpango wa siku zake, mzazi anampa nafasi ya kuamua, lakini humshauri jinsi ya kutumia muda vizuri. Pia mzazi anaposhirikiana na kijana kuandaa bajeti ndogo ya matumizi ya shule au burudani, humfundisha uwajibikaji wa kifedha.
iii) Kijana anaposhindwa katika michezo au mashindano, mzazi humfariji, kumtia moyo, na kumfundisha kujaribu tena badala ya kuacha.
Njia hii husaidia kujenga heshima, uelewa wa jamii, na uwezo wa kijana kukabiliana na changamoto za kila siku kwa njia chanya.

**8.1.4 Malezi katika Hatua ya Mpito kuelekea Utu Uzima**
Katika hatua hii, mtoto huanza kujitegemea na kujiandaa kwa majukumu ya utu uzima. Malezi yanapaswa kujikita katika ushauri, ufuatiliaji, na kukuza uwezo wa kufanya maamuzi yenye uwajibikaji. Mzazi awe mshauri na mwelekezaji zaidi kuliko mtawala.

Mifano:
i) Kijana anapochagua chuo au kazi, mzazi anashirikiana naye kwa kujadili fursa na changamoto, lakini anampa nafasi ya kufanya uamuzi wa mwisho.
ii) Kijana anapokuwa na uhusiano wa kirafiki au wa kimapenzi, mzazi anatoa ushauri juu ya maadili na hisia, akimruhusu kujifunza kutokana na matokeo ya maamuzi yake.
iii) Mzazi anaposhirikiana na kijana kupanga bajeti ya matumizi ya mwezi au kupanga muda wa kazi na burudani, humfundisha uwajibikaji na kupanga maisha.
Hii husaidia mtoto kuendeleza tabia ya uwajibikaji na kujitambua kama mtu huru lakini anayejali jamii.

Hitimisho; Malezi bora yanahitaji uelewa wa hatua tofauti za ukuaji wa mtoto na matumizi ya mbinu zinazofaa kwa kila hatua. Hakuna mbinu moja inayofaa kwa kila umri. Mzazi au mlezi anayebadilisha mbinu zake kulingana na ukuaji wa mtoto humsaidia mtoto kukua kiafya kimwili, kihisia, na kimaadili.
Safari ya malezi katika hatua hizi ni mchakato endelevu unaohitaji subira, maarifa, na kujifunza kila siku. Hii husaidia kumjenga mtoto anayewajibika sasa na kuwa mtu mzima mwenye mchango chanya katika familia na jamii.

**Tembelea**

**www.kitabumarket.co.tz**

**uburudike**

# K.O.K.W.A


**K.O.K.W.A**
**Mchezo mwingine mgumu mno ambao KAMANDA AMATA anakutana nao katika maisha yake ya UJASUSI.**

**Aisee hiki ni kionjo tu! Kula chuma hicho…!**

---

MVUA ya rasharasha ililifanya Jiji la Antananarivo kuwa chepechepe. Tope jepesi lilizijaza barabara zisizo na lami zilizokatisha kwenye viunga vyake. Hoteli ndogo ya Le Combava yenye hadhi ya nyota tatu ndiyo iliyomhifadhi Kamanda Amata kwa takribani saa 48 tangu awasili katika jiji hilo. Mara hii hakuja kustarehe na warembo wa Kimalagash bali alikuja kazini. Kazi iliyohitaji umakini na akili ya kiwango cha juu kuliko unavyofikiria. Hata yeye mwenyewe alilijua hilo na ndiyo maana hakutaka kabisa kupoteza hata nukta ya utimamu wake kwa mambo aliyoyaita kwa siku hiyo 'yasiyo na maana'.

Mchana huu alikuwa na kazi moja tu, kazi aliyopewa na bosi wake, Madam S. Kuhakikisha anaipata 'Kokwa'. Mpaka sekunde hiyo tafutishi zao zilionesha wazi kuwa Kokwa hiyo ipo Antananarivo na huko haitakaa muda mrefu kwani inapaswa kupelekwa pahala pengine. Hilo halikutakiwa kufanikiwa hata kidogo. Alipohakikisha amekamilika, alikuwa tayari kuingia mjini kukabiliana na adui yake. Kila kitu alishakiweka sawa. Kilichomsubiri ni utekelezaji tu. Akiwa ndani ya suti safi nyeusi, iliyotanguliwa na shati jeupe na tai ndefu nyeusi, alikuwa tayari kwa safari. Kofia nyeusi ya Kiyahudi akaipachika kichwani pake huku mkononi akiwa na fimbo ya mpingo iliyokuwa na nakshi nzuri za kupendeza.




Akatoka nje ya chumba chake na kuelekea mapokezi. Pale akaacha kadi ya chumba na kufuata maegesho ya hoteli hiyo. Aliliendea gari lake alilokodi kwa shughuli za hapo, Renault la kisasa kabisa lilikuwa likimsubiri. Akaingia na kutulia nyuma ya usukani. Katika nchi ya Madagaska, magari aina ya Renault na Citroen ni maarufu sana hivo na yeye akakodi moja ya aina hiyo. Kukodi gari hilo aina ya Renault hakukuwa kwa bahati mbaya bali ni

moja ya kufanya kazi zake kuwa rahisi zaidi awamo jijini humo. Akatia funguo na kuipa moto injini, kisha taratibu akayaacha maegesho na kuelekea kule anakokutaka.

Alikuwa makini barabarani kwani kuna kitu ambacho alikigundua siku hiyo. Hii ilikuwa siku yenye nyendo za tofauti kabisa kwa wakazi wa jiji hilo. Kwanza aliwaona wawili wawili, yaani kila alipo mwanaume palikuwa na mwanamke. Mavazi waliyokuwa wamevaa yalimwachia mswali mengi kiasi. Yalikuwa ya kitamaduni zaidi. Kuna nini leo? Akajiuliza. Lakini kwakuwa hilo halikuwa la msingi katika kazi yake, hakulitilia maanani. Akilini mwake alijaa mtu mmoja tu, Mikhail Planchikov. Huyu ndiye haswa aliyemfanya kijana huyu kufika Antananarivo. Kila kitu kilikuwa sawa, na sasa alikuwa anaelekea pahala alipo bwana huyo, Mzungu kutoka Russia, mtaalamu wa masuala ya nyuklia, aliyekuwa Tanzania kwa utafiti wa madini hadimu ya urani miaka takribani mitano iliyopita.
Le Louvre Hotel ndiyo haswa alipokuwa anahitaji kufika. Kwa mwendo wa taratibu, aliendesha katika Barabara ya Chinoise Saissoniere. Lakini, jambo hasilolitegemea alikutana nalo. Kizuizi cha askari wa usalama barabarani kuelekea Boulevard de L'Europe, barabara iliyokuwa sahihi sana kwake kufika pale anapotaka. Mmoja wa wale askari akalisogelea gari la Kamanda Amata pale liliposimama. Ilikuwa ni mita chache sana kutoka kwenye kile kizuizi.
"Samahani, unaelekea wapi?" yule askari kijana akamuuliza Amata baada ya kioo kushushwa.
"Le Louvre Hotel…" Amata akajibu kwa Kifaransa cha kubabaisha.
"Le Louvre Hotel… ok! Sasa itabidi ubadili njia, tumia Boulevard de L'Europe kuelekea Cathestudio… huko utapata maelekezo mengine," yule kijana akamuelekeza.
"Kuna nini mpaka mfunge barabara?" akauliza.
"Leo ni kilele cha sherehe ya Canival, hivo watu wengi watakuwa kwenye hii barabara usiku huu

## NAGUIB MAHFOUZ

*Inatoka ukurasa wa 18*

Katika safari yake iliyojaa mafanikio, Mahfouz alipokea tuzo za juu zaidi, kuanzia tuzo za kitaifa za Misri na Nishani ya Jamhuri, hadi Tuzo ya Nobel ya Fasihi mnamo mwaka 1988, na kuwa mwandishi wa kwanza wa Kiarabu kupata heshima hii ya kimataifa. Katika mwaka huo huo, alitunukiwa Qiladat Al-Nil Al-Uzma (Shanga ya Mto Naili).

Mnamo Agosti 30, 2006, Naguib Mahfouz alifariki dunia, lakini bado aliendelea kuishi katika dhamiri ya Waarabu, akiwa shahidi wa zama alizoziandika kwa wino wa uaminifu, na kuziunda kuwa fasihi isiyozeeka. Alikuwa mwana wa mtaa… akawa mwana wa ubinadamu.

Mwandishi huyu mashuhuri wa kimataifa, Naguib Mahfouz, anaongoza taswira ya kitamaduni kama Mhusika Mkuu wa Maonesho ya Kimataifa ya Kitabu ya Kairo katika toleo lake la 57, ambapo picha yake inapamba bango la maonesho hayo kama heshima kwa kiongozi wa kipekee wa fasihi aliyeunda dhamiri ya riwaya ya Kiarabu, na kuwakilisha kwa kina binadamu wa Misri katika mabadiliko yake ya kijamii na kiakili, hadi kazi zake zikafikia upeo wa ulimwengu.

Toleo hili linakuja kuthibitisha nafasi ya Mahfouz kama ishara ya ubunifu wa Kiarabu na sauti ya kibinadamu iliyovuka mvvvvveeeipaka ya kijiografia. Katika toleo la 57, "Di Bordo" anakuwa mgeni wa heshima, katika muktadha wa kuimarisha mazungumzo ya kitamaduni na kufunguka kwa tajriba mbalimbali za kifasihi na kiakili, jambo linaloimarisha nafasi ya maonesho haya kama daraja la kukutanisha tamaduni, na jukwaa kuu la kusherehekea neno na maarifa.

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (08)- Na: Eva Mrema

***Ilipoishia…***

**Kushoto kwake ni njia ya giza ambayo kwa karne hii hakuna aliyefanya jaribio la kuipita baada ya tetesi za mtalii wa Kizungu kupotelea huko akiwa na mbwa wake ambaye alipatikana miezi mingi baada ya kupotea huko nchini Kenya. Hadithi ya kutoweka kwa mzungu yule haijapata mwendelezo, hakupatikana yeye wala masalia ya mwili wake.**

***Endelea...***

Tuliogopa na kuchagua kuelekea kulia. Huko tuliona kiti cha enzi. Ni mfano wa kochi lililochongeka kistadi kutoka kwenye mwamba. Tulilikalia na kupiga picha. Tulitoka na kupanda ndege. Unacheka? Ndio kuna mahali wanasema kupanda ndege, tulipanda na baada ya dakika chache ndege ilitufikisha nje ya mapango yale makubwa. Tulishuka ngazi za ndege zilizojichonga vyema kutoka kwenye miamba. Nje kuna mijikamba minene sana ya miti iliyopafanya pavutie. Tulipiga picha za kutosha na hapo safari ya kuyatalii mapango ya Amboni ikatamatika kwa furaha.



Majira ya jioni yalitukuta muheza. Tuliyoyoma mdo-mdo hadi Magoroto. Tulipata mahala tulivu pa kupumzikia. Kuna chaguzi nyingi ila sisi tulichagua kusikiliza muziki uliopigwa kwa vyanzo vya asili. Wapigaji ni vijana wenye mionekano nadhifu na haiba ya muziki. Hapa hakukuwa na sauti za binadamu, zilisikika ala tu. Ngoma zilizowambwa kiufundi ziliiwamba vizuri jioni yetu. Mdogo wangu alionja ladha mpya ya maisha nje ya midundo ya kielektroniki. Alicheka vioja vya wacheza ngoma. Mimi na Sunche tulihangaika kubadili mikao iliyotusaidia kugandana kama ruba muda wote. Watoto wa mjini wanasema 'tulikuwa tuna enjoy'

Muhudumu aliyepewa jukumu la kutuhudumia sisi tu kama wageni maalumu yaani VIP, aliumudu sana uwanda wa ushawishi. Tulionja vyakula na vinywaji mbalimbali vyenye upekee wa aina yake. Majira ya saa nne usiku alitusanua kuwa kuna 'karaoke' upekee wa karaoke yao ni kwamba, wapo wapigaji wa vyombo vyote vya muziki, wapo waitikiaji wa kila wimbo, halafu chaguo ni la mteja kujiimbia au kuchagua mtu amuimbie. Nilimuomba Sunche akaniimbie japo kidogo. Alicheka na haraka tulijongea eneo la tukio kwa kukimbia kama watoto. Dogo alituchukulia kama sehemu ya burudani, alicheka utoto wetu mara zote. Alijipa kibarua cha mtunza kumbukumbu, alipiga picha kwa simu yangu. Ilikuwa na uwezo mkubwa na kamera nzuri.

Tulikuta bendi wanapiga muziki usio na muimbaji. Sunche alinivutia kiti, nikaketi, alinibusu na kunisisitiza nisiicheke sauti yake. Alitembea kwa haraka na kupanda jukwaani. Alijikohoza hali amekishika kipaza sauti. Hakuwa na sauti nzuri kwa wengine ila kwangu aliimba kwa sauti tamu kuliko wenye wimbo aliouimba. Na yeye kama mimi tu, alipenda nyimbo za kizungu. Sio kwa sababu ya asili; bali ujumbe ndani ya nyimbo husika. Hakuchukua muda jukwaani, aliimba ubeti wa kwanza na kiitikio cha wimbo wa ….. Beautiful in white, anajua urahibu wangu juu ya nguo nyeupe na hata usiku huu nilivaa gauni fupi jeupe. Nilimfuata na kumkumbatia, kabla ya kuketi aliniomba niimbe, amependa sana kuisikia sauti yangu. Nilipanda jukwaani kwa msaada wa mahabuba wangu. Najua wimbo anaoupenda sana Sunche wa kiswahili, akili iliniambia nimshtushe. Uliimbwa na mwanaume mwenye sauti nyororo sana, na mimi nikawasiliana na bendi niuimbe. Zilitangulia ala, ikafuata sauti yangu.

"Pendo langu, halina mwisho,..ooh Wewe ndio wangu, leo hata kesho ooh! Sogea, nikumbatie eeh! kwani najua huamini uko na mie eeh! Usilie, ufurahie..eh Mimi


**RIWAYA: NGUVU YA KIAPO**

Inapatikana katika kitabu (nakala ngumu) na soft copy (nakala tepe) kwa bei ya kirafiki.

**KITABU** - Tsh 10,000
**Dar es salaam:**

- Duka la Kona ya Riwaya - 0655428085
- Kalamu Tulivu Magomeni - 0718975659
- Posta Mpya kwa Joji - 0713454152
- Temeke kwa Eva Mrema - 0742630141

Soft Copy (Nakala tepe) PDF - Tsh 5,000
'Offer' kupitia Ngurumo ya Mwandishi ni - Tsh 3,000
Lipa kwa **MPESA LIPA NAMBA 36499709 Eva John Mrema**

## RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (08) - Na: Eva Mrema

sikuachi kamwe…eeeh eeeh.. eeeh Ulikuwa wimbo mpya mjini, aliimba muimbaji wa kitanzania niliyemkubali sana. Alijulikana kwa jina la Marlaw' uliitwa DAIMA NA MILELE. Sunche hakujizuia hata nukta. Alinifuata na kwa ushirikiano mkubwa nikaimba hali tunacheza kimahaba. Mdogo wangu alijikita kwenye kuchukua kumbukumbu. Niliimba na kila nilipokifikia kiitikio tuliimba wote sawia na bendi.
"Daima na milele eeh! Nitakuwa nawe..eeh Maisha yangu yoote……… Eeee..eeeh!"
Watu wote waliokuwepo eneo lile wakipata burudani walivutiwa mno. Wapendanao walituiga na kuanza kucheza pamoja. Wapweke walipiga makofi na kelele za kushangilia. Nikisema ulikuwa usiku mzuri naomba nieleweke, usiku ulikuwa mzuri sana.
Tulitoka pale hali tumechoka miili, tulielekea vyumbani. Mdogo wangu aliingia kulala na mimi na Sunche tuliingia kwenye ungwe ya pili ya usiku wetu. Tuliingia kukogeshana kwanza, eee, tulikogeshana kiasi kwamba msalani ulijichekea tu kwa namna tulivyokoga. Tulitoka tunachekacheka kama wajinga. Sunche alifungua jokofu dogo na kutoa mvinyo na bilauri mbili za kuunywea. Tuliketi na mataulo yetu kwenye kona ya chumba kulipowekwa viti viwili na stuli. Tuligonganisha glasi na mvinyo wa kwanza tukaubwia kwa pupa. Huu ni mchezo wetu siku ambazo tunataka kulewa. Tulivyoshusha glasi tulicheka mno. Tulipiga simu na kuagiza mvinyo wa zamani, wataalamu husema mvinyo wa zamani ni m'bora kuliko mpya. Haikuchukua japo dakika kumi, mvinyo ulitufikia mapema sana.

Tulizama kwenye unywaji uliochagizwa na nyingi soga. Sunche alinisimulia kisa alichokutana nacho mara tu alipohamia Tanzania. "Nilikutana na mwanamke mziki, baada ya kumlisha na kumnywesha akaanza kunifuata. Nilipoondoka, mwanamke alinifuata hadi garini na kutaka kwenda kulipa madeni. Nilijishauri na mwisho asili ikachukua nafasi. Nilimchukua na kumpeleka nyumba ya kulala wageni. Nilichukua kila tahadhari kuilinda afya yangu, nikasahau kulinda nguo wala pochi yangu. Asubuhi nilijikuta mtupu, niliibiwa kila nilichokuwa nacho. Sikuachiwa hata nguo ya ndani. Nililazimika kujifunga mashuka na kwenda kutoa taarifa kwenye uongozi wa nyumba ile ya wageni. Nashukuru funguo ya gari nilikabidhi mapokezi. Niliazimwa shuka, nami wala sikuwahi kulirudisha. Hili tukio lilinitoa imani na wanawake hadi pale ulipouvunja mwiko Tabita" Tulicheka sana.

Tuliendelea kuongelea maisha yetu ya utoto na ujana na baadae tukaanza kuipanga 'future' kilevi. Tulilewa kama tulivyotaka, vita ya maimai ikaanza, fujo zisizo na umwagaji damu zikaibuka, mimi na yeye ni wazuri kwenye mbio ndefu za pupa na fupi za kistaarabu. Tulitoshana. Kila mmoja aliichokoza silaha ya mwenzake kila alipohisi kuishiwa nguvu. Tulikomoana kwa hiyari kabisa.
Baada ya vita isiyotisha, tulilala kama mateja walioridhika na urahibu wao. Muda ulikimbia haswaa! Tuliamka saa tano, mwishoni kabisa mwa asubuhi kuelekea mchana. Kwakuwa nilimtumia ujumbe dogo wa kuchelewa kuamka, alipoamka alijiendea zake kufanya mazoezi kwenye gym ya kisasa iliyokuwepo hotelini pale. Kuamka na kuamka, mninginio wa ziada umetutawala. Tuliagiza supu ya kuku wa kienyeji na sharubati ya limao. Kama ilivyo ada, Magoroto walijitahidi kuhakikisha tunaufurahia uwepo wetu pale. Ukiagiza kitu kinakufikia ndani ya muda. Kabla ya chochote tulikunywa sharubati ya limao. Tukaingia kukoga na tuliporejea tukaivamia supu na kuinywa kwa pupa bila kuoneana haya. Tulijiweka sawa baada ya kupata staftahi tulivaa na kutoka nje ya malazi. Muda huo dogo tayari amepata marafiki wageni wa Kipalestina. Walikuwa wakiongea lugha ya kifaransa. Nilishangazwa mno namna mdogo wangu alitema ung'eng'e wa lugha hiyo adhim. "Sorry ccy nilisahau kukwambia nilijiongezea kozi ya Lugha, nikihitimu sheria, nitakwenda kupata astashahada yangu Ufaransa" dogo aliniambia na mimi kama mtu nisiye na maamuzi wala kauli juu ya chochote, nilimtazama Sunche. Alitabasamu, "Napenda watu wanaojiwazia mazuri na kuyachukulia hatua. Pambana, tukijaaliwa uhai, masomo yako Ufaransa yatadhaminiwa na mimi" weeh! Baada ya Sunche kusema hivyo nilimkumbatia na kumbusu shavuni, jambo hilo lilipelekea kila mja eneo lile acheke.

**BURUDIKA**
www.kitabumarket.co.tz

# KALAMU YANGU
## Kiroba Cheusi—Laura Pettie

Laura Paettie, mwandishi Bingwa wa Tuzo ya Nyerere ya Uandishi Bunifu msimu wa pili, katika toleo hili anaongea machache kuhusu kitabu chake kingine cha Kiroba Cheusi. Tuseme tu kwamba hiki ni kati ya vitabu bora sana vilivyoingia sokoni miaka minne iliyopita.
Huyu hapa yeye mwenyewe alipokutana uso kwa uso na mwandishi wetu...

**Katika Toleo lililopita, safuni hapa tulikuwa na mwanamama mahiri 'fundi mshona maneno' wa fasihi ya Kiswahili. Laura Pettie. Alitueleza mengi sana kuhusiana na kitabu chake cha DIRA YA MOYO. Basi, toleo hili pia bado naye na hapa anatueleza kuhusu kitabu chake kingine KIROBA CHEUSI.**

**Tueleze mantiki ya kuandika kitabu KIROBA CHEUSI, yaani kitu kitu Gani hasa kilikusukuma?**
**Laura:** Cha kwanza, nilitaka kuzungumzia aina za urafiki. Huwa ninaamini urafiki una nafasi kubwa sana kwenye maisha yetu ya kila siku, pasi na kujali hali zetu kiuchumi ama tofauti zetu kiimani. Kuna marafiki waliotujenga, waliotunafikia au waliotuporomosha. Nasi yawezekana tumefanyia hivyo wengine waliotuita marafiki. Kwamba, urafiki unaweza kuchangia kuinuka au kuanguka kwa mtu. Dhana ya urafiki katika Kiroba cheusi imeangazia mambo yote haya.

Pili ni dhana ya umasikini. Tunasema umasikini si kilema, lakini kuna mazingira yanaweza kumfanya mtu azunguke katika duara la umasikini maisha yake yote. Riwaya ya Kiroba Cheusi imechanganua hili kwa mapana. Unaona umasikini unavyotamba katika fikra, imani, matendo, mipango, mazingira na hata kauli za watu. Unagundua kumbe kuna wakati umasikini hauanzii au haupatikani kwenye kukosa pesa tu, kuna mizizi mingine ya kuangazia.

Tatu ni kuigusa mitazamo na hukumu za kijamii dhidi ya watu wa aina fulani. Nilitaka kuifanya hadhira itambue kuna watu tunawahukumu vikali, tunawaongezea udhalili na kuwatenga kwa sababu tu hatuwafahamu kwa undani. Hizi ni hukumu za kuangalia mwonekano wa mtu, mavazi yake, kipato chake, shughuli anayofanya ama elimu yake. Hizi hukumu zimetufanya tudhalilishe sana watu wanaohitaji faraja mno na kuwaabudu watu wanaostahili kuepukwa kabisa.

**Enhe, turudi kwa wahusika wa KIROBA CHEUSI, hebu tueleze, umefananisha na tabia halisi za watu waliokuzunguka au ni ubunifu tu?**
**Laura:**Nakiri naishi kwenye jamii yenye watu wanaofanania wahusika. Wengine ni watu wa karibu na wengine ni sehemu tu ya jamii ninayoishi. Kwa mfano, rafiki niliyeitabaruku riwaya hii kwake, ni mmoja kati ya watu wakarimu mno kama Morena. Mtu mwema sana.



LAURA 'PETTIE' KISSAKWA

Watu wa aina hii hawazaliwi kila siku, na hawapo kila mahali. Kuandika riwaya hii ilikuwa zawadi yangu kwake kuonyesha na kuthamini ipasavyo wema alionao. Kwa upande wa sehemu ya jamii, unaweza kuwa shahidi pia. Watu aina ya Ndeana, Tarik, Mzee Shata, Fatumata, Kimboka wapo sana tu. Kwa kifupi, kila mhusika nimemtoa kwenye maisha yetu ya kila siku.

**Wengi waliosoma kitabu Hiki wameshangazwa na uwasilishaji wako wa maisha ya mtaani. Wanajiuliza Laura kazijuaje tabia hizi za "kitaa"?**
**Laura:** Ni kweli. Maswali yenye mwelekeo huu niliyapata sana kitabu kilipotoka. Hata sasa kwa wasomaji wapya, wengi huniuliza umezijuaje tabia fulani? Umewahi kuishi uswazi? Hizi dhiki, kero, raha, imani za uswazi

wewe umezijuaje? Na kadhalika. Kusema ukweli, mara nyingi nilijitahidi kukwepa kujibu moja kwa moja. Nami nilikuwa najiuliza kwani naonekanaje hata watu waniulize hivi?

Unajua kuna namna fulani, sehemu kubwa ya jamii huwa inahisi mtu akisema hajawahi kuishi maisha fulani au hajawahi kuishi sehemu fulani, inachukuliwa kama anajikweza au anajiona bora. Wakati kiuhalisia ni kweli hajawahi kuishi hayo maisha ila ameishi maisha mengine ambayo ni ya kawaida kabisa, hayana ukubwa huo ambao mtu anaufikiria. Hii ilinifanya kuyakwepa haya maswali kinamna, mpaka baadaye sana nilipoanza kuona si vibaya nikisema sehemu kubwa ya uandishi wa Kiroba Cheusi ni ubunifu na utafiti.

Kwa mfano, kuna siku katika safari za hapa na pale, niliamua kupita  Vingunguti ndanindani huko, nikaingia barabara za mtaani palipochangamka, ili tu kupata picha fulani halisi zaidi. Mengine ni nguvu tu ya *imagination*. Ukishamaliza kuandika, unarudia kusoma, unajiuliza hiki ni kitu halisi kweli? Na hii si mara ya kwanza kuandika kitu ambacho sijakiishi. Hata hapo zamani, tena utotoni, nikiwa bado kinda katika uandishi, nilipata kuandika mahojiano ya mahakamani, nikaandika maisha ya nje ya nchi, vitu ambavyo nilikuwa sijawahi kuvizingatia au kuviishi.  Furaha yangu kubwa ni kuona nimeweza kuandika uhalisia unaoshangaza. Hili ni kubwa sana kwangu

**Na je; maoni Gani umeyapata kutoka Kwa wasomaji wa kitabu hiki?**

Pongezi nyingi mno. Nakumbuka mmoja wa wasomaji, Mwalimu Richard Mabala, aliniambia hii stori ni ya kipekee sana. Maoni yake yalinipa nguvu kubwa ya kutaka kuwa bora zaidi katika uandishi. Siwezi kusahau hili.

Kulikuwa na maswali ya kutaka kujua kwa nini nilichagua mwisho wa aina ile, yaani *Ambiguous ending* ambayo inamfanya msomaji kufikiri zaidi na zaidi.

Kuna waliotaka kujua uhalisia umetoka wapi? Kama nimewahi kuishi uswazi. Kuna waliotamani mhusika fulani asingefanya hivi au vile. Kuna waliorejea na maoni ya kuwa wamelia, wamecheka, wameogopa sana, na wapo waliojifunza kitu kuhusu tabia fulani, upande mwingine wa maisha, dhana potofu walizoamini na mengineyo. Pia, wapo walionipa maoni ya kitaaluma. Kwa kifupi, nilipokea maoni ya aina zote kwa moyo mkunjufu.






Oh, tena nisisahau, ndiyo kitabu kilichoniletea ripoti nyingi kutoka kwa wasomaji kuwa wameibiwa hiki kitabu.

**Asante sana Bi. Laura '72' kama mwenyewe unavyojiita. Naamini hata wale ambao bado hawajasoma kitabu hiki cha Kiroba Cheusi basa sasa watakuwa na hamu ya kukitafuta. Kinapatikana duka la Kona ya Riwaya Kinondoni.**

**Laura tunasubiri kazi yako nyingine ili tuburudike na kujifunza.**

## Tangazo




**Lini ?**

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com